

# UTANGULIZI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

Mwandishi: Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid

Mhadhiri wa Fiqhi Linganishi
Mkuu wa Kitivo cha Sheria ( Ujaji)
Chuo kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhamad bin Saud- Riyadh
Mwaka wa Kiislamu 1425

REFERENCE

COMITE INTERNATIONAL GENEVE
ICRC

# UTANGULIZI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

**Mwandishi: Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid**

**Mhadhiri wa Fiqhi Linganishi**
**Mkuu wa Kitivo cha Sheria ( Ujaji)**
**Chuo kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhamad bin Saud- Riyadh**
**Mwaka wa Kiislamu 1425**

Utangulizi wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu

Mwandishi: Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid

Kimesahihishwa na Sheikh Saidi Salim Saidi – Bawazir

© Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu

# YALIYOMO

**Haki miliki** **2**
**Dibaji ya Mwakilishi wa Kikanda Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu** **6**
**Utangulizi** **9**
Pekuzi ya kwanza 11
Utangulizi 12
Mosi: Vita katika mtazamo wa Kiislamu 13
Pili: Maana ya Sheria ya Umma ya Kimataifa katika Uislamu 15
Tatu: Msamiati wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu 22

**Pekuzi ya kwanza** **27**
Sehemu za utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu 28
Kulinda haki za majeruhi na waliokumbwa na majanga 28
Haki za mateka 29
Haki za watu waliopotea na maiti 36
Haki za raia 39

**Pekuzi ya pili** **45**
Utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu 46
Mazingatio ya kibinadamu yaliyopatikana katika Vita vya Badri 48
Mosi: Mazingatio ya kibinadamu yanayohusu namna Mtume (juu yake rehema na amani) alivyoishi na wanajeshi wake 48
Pili: Mazingatio ya kibinadamu juu ya namna Mtume alivyoishi na mateka 51
**Hitimisho** **59**

## BISMILLAAHIL RAHMAANIL RAHIIM

# DIBAJI

Ni fahari na utukufu mkubwa sana kwangu kupewa kazi ya kuandika dibaji la kazi hii ijulikanayo kama Utangulizi wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu ambayo inasimamiwa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu kupitia ofisi yake ya Kikanda iliyopo Uarabuni.

Kwa hakika, Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ina historia ndefu sana, ikianza tangu Mkataba wa Kwanza wa Geneva wa mwaka 1864 uliohusu kuboresha hali ya wanajeshi majeruhi waliodhurika vitani. Itakumbukwa kuwa katika kipindi ambacho ni zaidi ya karne moja na miaka thelathini kumewekwa mikataba tofauti ambayo imeweka sheria mbalimbali za kuwalinda wahanga wa migogoro ya kutumia silaha sambamba na kuwekwa kwa mipaka ya nyenzo na mbinu za vita. Historia hii iliendelea mpaka palipoanzishwa Mahakama ya Kudumu ya Makosa ya Jinai kama ilivyoelezwa katika Mkataba wa Roma wa mwaka 1998.

Mikataba yote hii imelenga kuzuia madhara ya vita, kwamba madhara hayo yasiwaguse watu wasiohusika au kugusa vyanzo vya huduma za kijamii. Na licha ya kwamba mikataba hiyo yote pamoja na ile ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inakubaliana kuhusu lengo moja tu la kulinda utu wa binadamu, ila tofauti pekee iliyopo kati ya mikataba hiyo ni kwamba Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu hutekelezwa katika nyakati za vita vya kutumia silaha tu peke yake, sawa sawa iwe ni vita vya kimataifa au vya ndani.

Misingi pamoja na maadili mazuri yaliyotajwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ndiyo sheria zile zile zilizoletwa na dini zote za mbinguni ambazo ni rehema kwa wanadamu. Lengo kuu la sheria hizo ni kumtukuza binadamu, kuzipa nafsi malezi bora, kuimarisha na kudumisha amani kwa wote.

Kwa hakika, kitabu hiki ambacho mimi ni mfunguzi wa dibaji lake, kimekuja kuonesha na kuimarisha misingi ya ubinadamu iliyopo ndani ya Sheria ya Kiislamu.

Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid, Mhadhiri wa Fiqhi linganishi katika Kitivo cha Sheria (Ujaji) na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhamad bin Saud, ndiye aliyejitolea kuandika kitabu hiki ambacho kimeelezea Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa kazi kubwa aliyoifanya ambayo imezaa matunda makubwa, nayo ni kupatikana kwa kitabu hiki ambacho kitakuwa ni mwongozo mzuri wa kuifahamu maudhui hii. Na kwa kuwa Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu tangu ilipoanzishwa mwanzoni mwa nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, ina desturi ya kuzihamasisha nchi juu ya kuikuza na kuiendeleza Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, sambamba na kusambaza kazi zilizoandikwa juu yake, bila shaka Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu itakuwa imefurahishwa na kazi ya mtunzi wa kitabu hiki ambapo imekichapisha kwa matarajio kwamba itakuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha na kueneza kazi za Kamati hii.

Ijulikane kwamba, Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu ambayo mimi ni mwakilishi wake kwa nchi za Uarabuni, ni taasisi inayotekeleza majukumu yake pasi na upendeleo au kuegemea upande wowote, pia ni taasisi huru inayojitegemea, ambapo nchi 191 wanachama wa taasisi hii zilisosaini Mikataba Minne ya Geneva ya mwaka 1949 na mikataba mingine miwili ya ziada ya mwaka 1977 wameipatia jukumu la kuwalinda na kuwasaidia wahanga wa migogoro ya kutumia silaha.

Na tangu hapo mwanzo, waasisi wa Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu waliona kwamba kuna umuhimu kwa taasisi hii kuwa na nembo yake maalum ya kimataifa ambayo itakuwa ni rahisi kuitambua, si kwa lengo la kuwalinda majeruhi wa vita tu peke yake, bali pia kuwalinda wale wote wanaotoa msaada kwa wahanga hawa pamoja na vitengo vya huduma za kimatibabu ikiwa ni pamoja na vitengo vya afya vya adui, ambapo wapiganaji watatakiwa moja kwa moja kuacha mara moja kuishambulia nembo hiyo na waiheshimu.

Mkutano wa kimataifa wa mwaka 1863 ndio ulioamua kwamba nembo ya Kamati hii iwe ni msalaba mwekundu ambao nyuma yake kuna rangi nyeupe -kinyume cha bendera ya Uswizi ambayo msalaba wake ni mweupe na nyuma yake kuna rangi nyekundu- ili iwe ni nembo pekee ya vikundi vya kuwasaidia wanajeshi majeruhi. Na baada ya kupita mwaka mmoja tokea kupitishwa maamuzi hayo, mkutano wa wanadiplomasia wa Kamati hii uliitambua nembo hii kuwa ni nembo pekee ya huduma za matibabu kwa wanajeshi, ambapo Mkataba wa Geneva wa mwaka 1864 uliithibitisha rasmi. Lakini ulipofika

mwaka 1876 utawala wa Ottoman uliamua kutumia mwezi mwekundu badala ya msalaba mwekundu (kinyume cha bendera ya utawala wa Ottoman) ambapo mwaka 1929 nembo hiyo ya mwezi mwekundu pia ilipitishwa kuwa ni nembo rasmi ya taasisi hii. Na kwa maelezo haya mafupi, imebainika kwamba mwezi mwekundu na msalaba mwekundu ambazo ni nembo maalumu kwa ajili ya kazi za kibinadamu hivi sasa, ni nembo ambazo hazina mahusiano yoyote na mambo ya kidini.

Mwisho wa utangulizi huu napenda kumshukuru tena Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid kwa kuandika kitabu hiki kilichosambazwa kwa ushirikiano na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu.

**Kuwait 2 Dhul Qaada 1425 Hijr sawa na 20/Dec/2004.**
**MICHEL MEYER**
**Mwakilishi wa Kikanda**
**Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu**
**Kuwait.**

# UTANGULIZI

Kadhia ya haki za binadamu katika kipindi cha migogoro ya kutumia silaha ni moja ya kadhia muhimu za hivi sasa ambazo zinasumbua vichwa vya wasomi na wanafikra, ni kutokana na madhara yanayowakumba wanadamu yanayosababishwa na vitendo vya kiadui, dhulma na vita.

Kadhia hii inabeba umuhimu mkubwa sana, hasa katika zama hizi za sasa zijulikanazo kama zama za ustaarabu, kwani mambo yaliyotokea katika miji ya Hiroshima na Nagasaki nchini Japan, miji ya Sabra na Shatila nchini Lebanon, mjini Halibja nchini Iraq, Bosnia na Herzegovina, Kosovo na Kashmir, Chechnya, Jenin Palestine, pamoja na majanga yaliyotokea Iraq na yale ya mji wa Rafah Palestina, na matukio mengi yasiyokuwa hayo yanamfanya mtu ashangae na kujiuliza: Ziko wapi sasa haki za binadamu?

Vita ndivyo humfanya mtu asahau ubinadamu wake, maadili na hata tabia nzuri, na vita (kwa ushahidi wa kihistoria) ndio tukio kubwa sana linaloshusha maadili na misingi ya kibinadamu, kwa sababu wakati wa vita huvunjwa sana haki za binadamu, na ndipo binadamu huyu aliyetukuzwa hukosa hadhi na thamani yake. Haya ndiyo yanayopelekea kwamba kuna umuhimu kwa wasomi na wadau kutafuta njia za kupambana na hali hii pamoja na kuidhibiti kwa namna ambayo italinda misingi ya kudumu ya kibinadamu.

Kwa msingi huo, kitabu hiki (licha ya kwamba ni kidogo) kimejikita katika kuzielezea haki za binadamu kwa mtazamo wa Kiislamu katika kipindi cha migogoro ya kutumia silaha, au Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu. Pia kitabu hiki kimejikita katika maandiko ya kisheria na maono ya wanazuoni wetu, kama ambavyo kimenukuu kutoka katika vitabu vingi vya kisasa. Tegemeo letu ni kwamba kitabu hiki kitakuwa ni msingi mzuri wa maudhui hii kwa yeyote atakayeandika hapo baadaye.

Ijulikane kwamba, ibara hii "Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu" ni msamiati mpya, ijapokuwa unajulikana unalenga nini, hivyo basi, katika pekuzi za kiislamu wanazuoni wa Sheria huwa wanatumia neno (Al-Siyar wal Maghaazi) kwa maana ya (Mwenendo au Vita) ambalo huwa linamaanisha Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu. Kwa upande wake Imam Sarkhasy amefafanua katika kitabu chake Al-Mabsout sababu ya jina hilo akisema: Neno (Siyar) la Kiarabu-ni wingi wa neno Sira, (ambalo maana yake ni mwenendo) na ndiyo maana

mlango huu ukaitwa hivyo, kwa sababu ndani yake hubainishwa mwenendo wa waislamu juu ya kuishi na wapiganaji wasiokuwa waislamu pamoja na wale waliochukua ahadi kwa waislamu kwamba wapo tayari kuhukumiwa kwa sheria ya Kiislamu, pia huelezwa namna ya kuishi na wale wanaofikia katika ardhi ya waislamu lakini hawakai hapo makazi ya kudumu, pamoja na wale wanoishi katika ardhi ya waislamu kwa kulipa kodi. Kisha akasema Sarkhasiy: Mlango huu umeitwa Al-Maghaazi (neno la Kiarabu ambalo linamaanisha vita) kwa sababu misingi yake inatokana na mwenendo wa vita vya Mtume (juu yake rehema na amani). Imam Muhamad bin Hassan Ash-Shaybaniy ametunga kitabu kiitwacho (Al-Siyar), kitabu hiki kimeshereheshwa na Imam Sarkhasiy katika juzuu tano, maudhui ya kitabu hiki ndio maudhui inayojulikana leo kama (Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu) maudhui hii kwa upande wa waandishi wa kisasa wa mambo ya kisheria imejulikana kwa jina la (Sheria ya Vita au Sheria ya Migogoro ya Kutumia Silaha).

Kuenea kwa haraka kwa msamiati au istilahi hii ya mwisho, kulipelekea msamiati huo kupewa fasili na kuandikwa katika vitabu vya hivi karibuni, hivyo, kutumika rasmi katika mikutano ya kimataifa na ya nchi mpaka ikazoeleka.

Na licha ya kwamba pekuzi hii itabaki kuwa ni dondoo tu juu ya maudhui hii ila mwandishi atatumia njia ya uchambuzi yakinifu ili kujaribu kupata picha ya ujumla ya maudhui hii au kuweka misingi ambayo yumkini ikawa ni mwongozo kwa tafiti pana zaidi zijazo.

Tafiti hii ina wigo wa zama na maudhui, wigo wa zama ni kwamba tafiti hii inajadili sheria zinazotekelezwa nyakati za migogoro ya kutumia silaha, na wigo wa maudhui ni kwamba inajadili sheria zinazolinda mali, sehemu na watu ambao hawana mahusiano yoyote na shughuli za kivita.

Na Utangulizi huu una mada zifuatazo:

- Vita katika Uislamu
- Maana ya Sheria ya Umma ya Kimataifa katika Uislamu
- Msamiati wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu.

**Pekuzi ya kwanza:** Medani za Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika Uislamu
**Pekuzi ya pili:** Utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu (hapa tutatumia Vita vya Badri vikiwa ni mfano wa utekelezaji huu).

**Hitimisho**

Mwisho, napenda kumshukuru Mat-ab Salehe Al-'Aashyawi (PhD) mhadhiri msaidizi wa sheria ya kimataifa katika chuo cha Diplomasia kilichopo chini ya wizara ya mambo ya nje, pia napenda kumshukuru ustaadh Sharif Atlam mratibu wa kikanda kitengo cha huduma za ushauri kwa ukanda wa Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika -Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu- kwa kuweza kusoma kitabu hiki na kutoa maoni muhimu ambayo tumeyapokea kwa mikono miwili.

Namuomba Mwenyezi Mungu anipe tawfiki na usawa katika kazi hii, na rehema na amani zimfikie Mtume wetu Muhammad.

12/06/1425
Profesa Zaid Abdel Karim Al-Zaid
Mhadhiri wa Fiqhi linganishi
Mkuu wa Kitengo cha Sheria (Ujaji)
Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Imam Muhamad bin Saud
Riyadh
Email: azzaid77@hotmail.com

# UTANGULIZI:

**Mosi:** Vita katika mtazamo wa Kiislamu
**Pili:** Maana ya Sheria ya Umma ya Kimataifa katika Uislamu
**Tatu:** Msamiati wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu.

# MOSI: VITA KATIKA MTAZAMO WA KIISLAMU

Asili ya mahusiano kati ya Umma wa Kiislamu na mataifa mingine ni kuishi kwa amani, Mwenyezi Mungu anasema "***Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu...***" (2:208)

Kuna baadhi ya watu ni vigumu kuishi nao kwa utulivu na amani, kwa sababu huwa hawataki kuheshimu sheria. Pia kuna baadhi ya watu au nchi fulani huwa zinahadaika kwa nguvu walizokuwa nazo zikilinganishwa na udhaifu wa jirani zao, nchi hizo hutenda vitendo vya dhulma na kuwaweka wenzao katika ukoloni. Hivyo basi, hakuna ubaya kutungwa sheria za kuruhusu kutumia nguvu ili kuwahofisha wanaodhulumu na hivyo kuimarisha amani, uhuru na uadilifu. Kwa kuzingatia msingi huu Uislamu umefaradhisha kupigana vita. Na lengo pekee la vita katika Uislamu ni kulinda haki za binadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema,
***"Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda." (8 :39)***

Kwa kigezo hicho, punde tu adui atakapoacha dhulma na kuwaacha watu wafuate dini zao itakuwa haifai kumpiga vita. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu, "***...Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu.*** "

Kutokana na maelezo hayo yaliyotangulia, imebainika kwamba Uislamu umefaradhisha vita kwa ajili ya:

**(a)** Kumzuia mtu aliyeanza uadui asiendelee na uadui huo, au,

**(b)** Kuitetea haki thabiti iliyoharibika kutokana na adui kuivunja, au,

**(c)** Kwa ajili ya kuimarisha usalama wa njia na uhuru wa dini na kumuwezesha yule anayetaka kuingia katika dini aingie pasi na kukumbana na vikwazo kutoka kwa mtu yeyote. Kanuni kuu ya kufahamu aya za Qur'an zinazozungumzia vita ni kwamba, endapo utakutana na aya yoyote ya Qur'an inayoamrisha kuuwa wale ambao si waislamu, aya hiyo inatakikana ifahamike kutokana na mtiririko wa maneno yaliyotangulia, ukirudi nyuma ya aya hiyo na kuzisoma aya zote kikamilifu utaelewa kwamba anayeelezewa hapa ni yule aliyetajwa katika aya zilizotajwa kabla ya aya hiyo, kwamba huyu ndiye anayekusudiwa kupigwa vita.

Pamoja na yote bado panatikiwa kuzingatiwa maadili na tabia nzuri wakati wa vita, kwani katika Hadithi iliyopokewa na Sulayman bin Buraydah, naye kapokea kutoka kwa baba yake, amesema: 'Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu pindi anapomteua mtu kuwa Mkuu wa Majeshi au Kikosi, akimuusia kheri, katika yale ambayo huwa anaiusia nafsi yake na anayowausia waislamu walio pamoja naye, kisha huwa anasema:

*"Piganeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, katika njia ya Mwenyezi Mungu, mpigeni mwenye kumpinga Mwenyezi Mungu, piganeni vita, wala msiibe mali, msivunje ahadi, msikatekate maiti, wala msiue mtoto mdogo, na ukikutana na maadui zako katika washirikina wape hiari ya mambo matatu, wakichagua jambo lolote kati ya hayo  wakubalie na usipigane nao, -kwanza- walinganie waingie katika Uislamu wakiupokea Uislamu wakubalie na usiwapige vita, na uwaambie kwamba wakikubali kuingia katika Uislamu basi na wao watakuwa na haki zote ambazo wanazo waislamu Muhajirina pia wana wajibu na majukumu yote ambayo yapo juu ya Muhajirina, wakikataa, basi – la pili- ni kuelekea huko basi waambie wao watakuwa kama mabedui wa kiislamu, kwamba, hukumu ya waislamu inayotekelezwa kwa waislamu ndiyo hukumu hiyo hiyo itakayotekelezwa kwao, na wala hawatapata chochote kitokanacho na ngawira au tozo, lakini watastahiki malipo hayo endapo tu wataungana na waislamu kupigana vita, wakikataa hilo nalo, basi -tatu- waambie watoe jizya nayo ni tozo, wakikubali kutoa wakubalie na usipigane nao. Wakikataa yote hayo basi omba msaada kwa Mwenyezi Mungu na upigane nao, na endapo utawaweka vizuizini watu wa ngome yoyote wakakutaka uwape dhima na ahadi ya Mwenyezi Mungu na dhima ya Mtume wake, basi usikubali kuwapa dhima ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume wake, lakini wape dhima yako wewe na jamaa zako, kwani nyinyi mkivunja dhima zenu ni jambo jepesi kuliko kuvunja dhima ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na endapo mtawaweka kizuizini watu wa ngome fulani wakakutaka uwasimamishie hukumu ya Mwenyezi Mungu basi usiwasimamishie hukumu ya Mwenyezi Mungu, bali wape hukumu yako, kwani wewe hujui kama ukiwawekea hukumu ya Mwenyezi Mungu utapatia au laa.*

Mwongozo huu unatoa mtazamo wa kiislamu wa ujumla katika kupigana vita, kisha unabainisha ni kiasi gani waislamu wanatakiwa kuwa na tabia njema katika kuishi na kutaamali na adui tangu mwanzoni mwa miale ya mwanzo ya kutangazwa kwa vita. Na hili ndilo lengo la kifungu hiki.

# PILI: MAANA YA SHERIA YA UMMA YA KIMATAIFA KATIKA UISLAMU

Sheria ya Umma ya Kimataifa hufasiriwa kuwa ni mjumuisho wa sheria tofauti zinazopangilia mahusiano ya wadau wa sheria ya kimataifa, katika hali ya amani na vita.
Tangu hapo kale, misingi mikuu ya Sheria ya Umma ya Kimataifa ni mikataba ya kimataifa, desturi pamoja na sheria na misingi ya pamoja ambayo imekubalika kimataifa, kama vile msingi unaotambua kwamba, mwenye kutenda jambo lolote la madhara basi atawajibika kwa madhara hayo, na kama vile misingi ya kuheshimu mikataba na makubaliano.

Kwa ujumla hii ndiyo misingi ya sheria ya umma, ama kwa upande wa Uislamu, tunaona kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliasisi dola ya kwanza kabisa ya Kiislamu katika mji wa Madina, ambapo alisaini mikataba ya kuishi kwa amani na nchi zilizomzunguka, lakini pia aliishi vizuri na majirani zake, pia palianzishwa mahusiano tofauti kati ya Dola ya Kiislamu na nchi hizi jirani, jambo ambalo lilipelekea ulazima wa kutunga sheria za kudhibiti mahusiano haya. Ni kusema kwamba, katika mtazamo wa kiislamu sheria hizi ni sawa na Sheria ya Umma ya Kimataifa.

Kwa muktadha huu, Sheria ya Kimataifa ya Kiislamu inaweza kufasiliwa kuwa ni mjumuisho wa sheria tofauti za kiislamu ambazo ni lazima kwa nchi za kiislamu kuzitekeleza katika mahusiano yake na nchi nyingine au taasisi za kimataifa.

Misingi muhimu ya sheria ya kiislamu ni:

1. **Umoja wa kibinadamu:** Sheria ya Kiislamu inawazingatia watu wote kuwa ni umma mmoja unaounganishwa na sifa moja tu, nayo ni kwamba wote ni binadamu, ama tofauti za utaifa na ukabila, hizo zipo tu kwa ajili ya kufahamiana na kushirikiana, na si kwamba jamii fulani ni bora kuliko jamii nyingine. Kwani ubora wa mtu hupimwa kwa kiasi cha utiifu wake wa kufuata maelekezo ya Mwenyezi Mungu mtukufu. Anasema Mwenyezi Mungu ***"Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume***

***na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi…"* (49:13)**

2. **Kushirikiana:** kushirikiana na kusaidiana katika mambo ya heri ni msingi ambao una nafasi kubwa sana katika Uislamu, anasema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"…Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui….." (5:2)***
3. **Kusameheana:** Sheria ya kiislamu imewataka waislamu kuwa na tabia ya kusameheana, anasema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"…Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu atapo leta amri yake…"*** (2:109) na akasema pia ***"…na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu…"*** (3:134) na akasema ***"Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (41:34)***
4. **Uhuru wa dini:** Sheria ya Kiislamu imeruhusu uhuru wa dini na imekataza mtu kulazimishwa kuingia katika dini ya Kiislamu, Mwenyezi Mungu mtukufu amesema ***"Hapana kulazimisha katika Dini…." (2:256***) Bali Dola ya Kiislamu inawalinda na kuwahami ambao si waislamu watakapoomba msaada kwa waislamu, na Uislamu unakataza kumlazimisha yeyote kati yao kuacha dini yake na kuingia katika Uislamu.
5. **Uadilifu:** Sheria ya Kiislamu imewataka wafuasi wake kufanya uadilifu katika hali ya amani na vita, kama ambavyo imewataka wafuasi wake kujitahidi kweli kweli kufanya uadilifu kwa watu wote, Mwenyezi Mungu mtukufu anasema, ***"Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu…" (4:135) na "…Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu…." (5:8)***
6. **Kutendeana kwa wema:** Uislamu unatambua msingi wa kutendeana jambo kwa wema kama njia ya kulipana, kwa sharti kwamba kutendeana huku kuwe na msingi wa tabia nzuri, na ikitokea kwamba kutendeana huku kutapelekea kutofanya uadilifu au kuvunja misingi ya maadili, hapo haitafaa kulipa jambo hilo, kwa mfano adui akitoza kodi batili ambayo inaziteketeza mali za waislamu, au endapo adui atavunja heshima ya baadhi ya waislamu, hapo haitafaa kwa waislamu kulipiza matendo kama hayo, vivyo hivyo haifai kwa muislamu kuongopa kwa mtu aliyemuongopea, au kumfanyia hiyana yule aliyemfanyia yeye hivyo. Wanazuoni wanaeleza sababu ya waislamu kukatazwa kulipiza mfano wa mambo hayo kwa dola kwamba, wale wasiokuwa waislamu wanapofanya hayo huwa wanavunja

amani, lakini sisi hatufai kuvunja amani, pia kufanya hivyo ni dhulma na sisi hatufai kufanya dhulma, ni kwa sababu tumekatazwa kufanya matendo ya kipuuzi hata kama adui atafanya hivyo.

Misingi mikuu hii inatokana na maandiko ya Qur'an na Hadithi za Mtume na desturi maalumu. Kuna maandiko mengi sana ya kisheria yanayozungumzia mahusiano ya Dola ya Kiislamu na mataifa mengine, kwa mfano:

- Mwenyezi Mungu anasema ***"Enyi mlio amini! Timizeni ahadi..." (5:1)***. Andiko kama hili huwa linafahamika hivi hivi kwa upana wake, kwamba waislamu wanatakiwa kutekeleza ahadi zote wanazotoa, na miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuheshimu mikataba inayosainiwa kati ya nchi na nchi. Hili ni andiko la kisheria la kiislamu ambalo linaiamrisha dola ya kiislamu kutekeleza ahadi katika mikataba iliyoingia na nchi nyingine.
- Kwa upande mwingine, kuna maandiko kadhaa yanatahadharisha kuhusu uhaini, Mwenyezi Mungu anasema "...Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi makhaini." (8:58) pia anasema ***"...Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye khaaini, mwenye dhambi." (4:107)*** hivyo basi Mwenyezi Mungu hapendi aina zote za uhaini, iwe ni uhaini wa kati ya mtu na mtu au kati ya nchi na nchi, bali uhaini unaofanywa kati ya nchi na nchi ni mbaya sana, na Mwenyezi Mungu anauchukia zaidi kwa sababu unawagusa watu wengi zaidi.

- Pia kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema, *"Dalili za mtu mnafiki ni tatu: akizungumza husema uongo, na akiweka ahadi huitengua, na akiaminiwa hufanya uhaini"*. Kwa msingi huu, muislamu wa kweli haongopi katika maongezi yake, wala hatengui ahadi yake na wala hamfanyii uhaini yeyote yule aliyemuamini awe ni adui au rafiki, nchi au mtu mmoja mmoja.

Maandiko kama hayo yapo mengi sana, na inatakiwa yafahamike vile vile kwa upana wake ambao unakusanya mahusiano kati ya mtu na mtu, sambamba na mahusiano kati ya Dola ya Kiislamu na nchi nyingine. Ufahamu huu unachagizwa na utekelezaji wa kivitendo uliofanywa na Mtume (juu yake rehema na amani) na mikataba yake iliyosainiwa kati yake na Mayahudi wa mji wa Madina, Maqureishi wa Makka ambao hawakuwa ni waislamu pamoja na Wakristo wa mji wa Najrani. Pia ufahamu huu unaonekana katika wosia

na nasaha mbalimbali ambazo Mtume aliwasihi viongozi wake wa jeshi waliopelekwa vitani.

**Na kuhusu desturi:** Kuna maandiko kadhaa yanayotambua desturi, maandiko hayo ni muendelezo wa maelezo yaliyotangulia hapo juu ambayo yameweka misingi ya mahusiano ya kimataifa kati ya Dola ya Kiislamu na nchi nyingine, kama:

1. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ***"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema..." (7:199)*** anasema Al-Qadhi bin Atwiya, neno 'na amrisha mema' maana yake ni kwamba uamrishe mema ambayo watu wanayajua na hayapingani na sheria. Imam Shatiby naye kwa upande wake anasema-hapo zinakusudiwa–(ada na desturi zilizozoeleka ambazo zinatakiwa kutambulika kisheria) na Sheikh Al- Sa'ady anatilia mkazo maana hii kwa kusema (ada na desturi ni msingi mkubwa ambao huwa ni marejeo ya masharti mengi na haki ambazo hazijatajwa kisheria wala kimatamshi)

2. Na anasema tena Mwenyezi Mungu katika andiko lingine la Qur'an ***"... Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini..." (22:78)*** hivyo basi, kuwazuia watu jambo ambalo wameshalizoea ni kuwapa tabu. Anasema Sarkhasy 'Katika kuacha ada ya wazi kuna tabu ya wazi' na kama ambavyo ada na desturi vinazingatiwa katika mahusiano kati ya mtu na mtu, vivyo hivyo vinazingatiwa katika mahusiano ya nchi na nchi katika mazingira tofauti, endapo tu ada na desturi hii havipingani na andiko la kisheria. Hii ndiyo sababu inayofanya tuseme desturi za kimataifa tunazozishuhudia leo duniani zina mazingatio maalum katika sheria, bali Dola ya Kiislamu itatakiwa kuheshimu na kutekeleza ada na desturi ambayo haipingani na Sheria ya Kiislamu, sawasawa desturi hii iwe katika Sheria ya Umma ya Kimataifa au katika moja ya matawi yake kama vile Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ambayo ndiyo mada yetu kuu katika kitabu hiki.

Pamoja na vyanzo hivi vya kisheria ambavyo ndio msingi wa Sheria ya Kimataifa ya Kiislamu, ila pia kuna upande mwingine muhimu unaopanua zaidi wigo wa utekelezaji wa sheria ya kimataifa nao ni kuzingatia tabia njema. Jambo hili la kuzingatia tabia njema liko wazi sana katika nyanja za Sheria ya Kimataifa ya Kiislamu, tena lipo katika kiwango kimoja, hakuna tofauti katika kutekeleza hili kati ya mahusiano ya kimataifa na mahusiano ya mtu mmoja mmoja. Hivyo basi kama ambavyo inatakiwa kuzingatia tabia njema kati ya

mahusiano ya mtu na mtu pia inatakiwa kuzingatia tabia njema hizo kati ya Dola ya Kiislamu na nchi nyingine, na kauli mbiu ya Sheria ya Kiislamu katika jambo hili ni kwamba haikubaliki kabisa kwamba kitu fulani kiwe ni haramu kwa mahusiano ya mtu na mtu kisha kitu hicho hicho kiwe ni kizuri tena ni halali na chenye kukubalika kwa mahusiano kati ya Dola ya Kiislamu na nchi nyingine katika mazingira fulani.

Kutokana na maelezo hayo imeeleweka kwamba miongoni mwa misingi ya Sheria ya Kimatifa ya Kiislamu ni kuzingatia tabia njema, na Dola ya Kiislamu inapaswa haswa kuzingatia msingi huu tena katika mazingira yote ya mahusiano yake na nchi nyingine pamoja na raia wao, hata kama itapelekea kwa Dola ya Kiislamu kulipa gharama kubwa na kukosa masilahi kemkem kwa kulitekeleza hilo, kwa sababu katika mtazamo wa kiislamu, kushikamana na tabia nzuri ni kitu chenye thamani kubwa sana kuliko kitu chochote, na jambo lolote litakalohitajia kujitolea ili kuhakikisha utekelezaji wa tabia njema, litahesabika kuwa ni kitu kidogo, na kinyume chake, kuacha kushikamana na tabia njema ni dosari mbaya ambayo haifutiki kwa chochote.

Hivyo basi, kama ambavyo Uislamu unaangalia upande wa haki za binadamu kwa jicho la kisheria, basi pia unaangalia haki hizo kwa wigo mpana zaidi wa kimaadili na tabia nzuri, na ushahidi juu hili ni kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema: *"Bila shaka nimeletwa kuja kutimiza tabia nzuri" (Muwatwa, Imam Malik uk 651).* Ujumbe huu muhimu ambao umekusanya risala ya utume katika tabia nzuri unaakisi nafasi ya tabia nzuri katika Uislam. Pia Uislamu unazizingatia tabia nzuri kwamba zina mahusiano makubwa na imani, kwani imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah (Mungu amuwie radhi) amesema, amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) *"Muumini ambaye imani yake imekamilika zaidi ni yule mwenye tabia nzuri zaidi"* (Sunan At-Tirmidhi).

Na tabia nzuri zina nafasi ya kipekee ambayo humfanya muumini awe karibu na Mtume (juu yake rehema na amani) kwani Mtume (juu yake rehema na amani) anasema: *"Hakika katika watu ninaowapenda sana kati yenu, na ambao watakuwa karibu zaidi nami siku ya Kiama ni wale wenye tabia nzuri zaidi"* (Sunan At-Tirmidhi). Hivyo basi mtu ambaye atakuwa karibu zaidi na Mtume (juu yake rehema na amani) siku ya kiama ni yule mwenye tabia njema, na kila muislamu anapokuwa na tabia njema zaidi ndipo anapojiweka karibu zaidi na Mtume.

Na muda mwingine tabia nzuri huwa zina daraja kubwa kuliko hata amali njema, mwongozo wa hili unapatikana katika hadithi iliyopokewa na Bi Aisha -Mungu amridhie- kwamba amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akisema: *"Hakika, muumini atapanda daraja kwa sababu ya tabia yake nzuri mpaka kufikia daraja ya mtu mwenye kufunga na kusimama usiku kwa ibada" (Sunan Abu Dawud).*

Miongoni mwa viashiria vya maadili mema ndani ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ni kushikamana na uadilifu katika mazingira yoyote yale, hata kama adui atakuwa ni mbaya kiasi gani, kwani Mwenyezi Mungu anasema ***"... Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda." (5:8)***

Maana ya aya hii ni kwamba, musiwafanyie uadui watu fulani eti kwa sababu tu wao wamekufanyieni uadui, lahasha, kwani muislamu anatakiwa ashikamane na maelekezo ya Mwenyezi Mungu na afuate njia ya uadilifu hata kama atadhulumiwa na kufanyiwa uadui. Kwa muktadhaa huu, haifai kwake yeye kumuongopea aliyemuongopea au kumfanyia hiyana mtu aliyemfanyia yeye hiyana. Uislamu umeenda mbali zaidi katika suala zima la uadilifu na kutaka kumuwajibisha mwenye kutenda kosa tu peke yake pasi na kumdhuru mtu mwingine, ni kwa sababu katika Uislamu haifai mtu kubeba kosa la mtu mwingine, Mwenyezi Mungu anasema, ***"Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine...." (35:18)*** ni kwamba kila mtu atabeba kosa lake, lakini inasikitisha kwamba mara nyingi msingi huu huwa unasahaulika pale kunapozuka vita au migogoro, ambapo wananchi hubeba makosa ya baadhi ya watu wengine, na hili hupelekea mauaji ya kimbari na mfano wake, hayo yote ni matokeo ya kuwabebesha makosa watu wasiohusika.

Na katika utekelezaji wa yaliyoelezwa hapo juu, imethibiti kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliwawajibisha wale tu aliosainishana nao mikataba kisha wakaivunja pamoja na wale walioshiriki na kuridhia ukiukwaji huu, ama wale ambao hawakutengua ahadi zao wala hawakuridhia hilo, basi Mtume (juu yake rehema na amani) aliwatekelezea ahadi yao kama ilivyokua.

Na kwa kupitia maneno ya wanazuoni wa sheria ya kiislamu wa madhehebu tofauti tunaweza kupata ufahamu huu, kwani Ibn Qudamah anasema katika kitabu chake Al-Mughniy: 'na yule ambaye hakutengua ahadi akimpinga

na kumkatalia mwenye kutengua ahadi kwa kauli au kitendo cha wazi au akajitenga naye au kumuandikia kiongozi wa kiislamu kwamba mimi napinga haya anayotenda huyu mwenye kutengua ahadi na nitaendelea kutekeleza ahadi yangu kama ilivyo, mtu huyu haki yake haitaguswa, bali kiongozi wa kiislamu ataamrisha mtu huyu awekwe mbali na mtenguaji na asiguswe kwa ubaya wowote, ili awajibishwe yule mtengua ahadi peke yake, na kama atakataa kutengwa au kumkabidhi mtengua ahadi -kwa kiongozi wa kiislamu- hapo hata yeye atahesabika kuwa ni mtengua ahadi  kwa sababu ya kuzuia kupatikana kwa mtenguaji'.

Hii inaonesha ni kiasi gani Uislamu unasisitiza kutekeleza ahadi na kufanya uadilifu, na ni kiasi gani unashikamana na maadili na kushikamana na kutekeleza ahadi.

Kitu pekee ambacho Sheria ya Kimataifa ya Kiislamu inatofautiana na sheria nyenginezo na kinaifanya iwe inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa ni kwamba misingi hii ya kidini humfanya muislamu awe anajilinda na kujipeleleza yeye mwenyewe, hivyo kumfanya atii sheria, ni kwa kuwa sheria hizi zinatoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo yeye anafanya hivyo kwa kumpenda Mungu wake huku akitaraji thawabu zake na kuogopa adhabu yake ambayo ameiahidia malipo kwa siku ya Kiama kwa mwenye kwenda kinyume na maamrisho  yake licha ya mateso ya hapa duniani. Kwa upande mwingine hizi sheria za kidunia mtu huzitii kwa kuogopa adhabu ya kidunia tu lakini sio kuiogopa misingi yake, na kwa mnasaba huu Abul Hayy Hijaziy (PhD) anasema 'ni jambo kubwa na zuri sana mtu kuitekeleza sheria kwa kuipenda tu, kwa sababu uhakika ni kwamba mtu hutii sheria kwa kuogopa adhabu na si kwa kuipenda, basi namna hii hii watu utawatoka uoga ule kidogo kidogo mpaka itafikia kwamba hawaiheshimu kabisa sheria yenyewe'.

# TATU: MSAMIATI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

Kwa kuwa ni vigumu sana kukomesha madhara ya vita yasiwepo kabisa, imelazimika kufanya kila liwezekanalo ili kupunguza madhara hayo ili yawaguse wahusika wanaoshiriki mapigano tu pasi na kuwagusa watu wengine wasiohusika, na huu ndio msingi wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu.

Na sheria hii ambayo inalenga kulinda haki za binadamu nyakati za migogoro ya kutumia silaha imeitwa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ili iwe na taswira ya ubinadamu. Hata hivyo inajulikana kwamba chimbuko la Sheria hii ya Kimataifa ya Kibinadamu ni hisia za kibinadamu zinazolenga kumlinda binadamu mwenyewe dhidi ya uadui katika nyakati za migogoro ya kutumia silaha.

Hivyo basi, Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ni tawi maalumu la Sheria ya Umma ya Kimataifa, na sheria hii pamoja na ile Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ni matawi mawili ya sheria yanayojitegemea kati ya matawi mengi ya Sheria ya Umma ya Kimataifa, na kwamba kila moja kati ya sheria mbili hizi ina nyanja na zama zake za matumizi. Ni kwamba, wakati Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inatumika nyakati za migogoro ya kutumia silaha, Sheria ya Kimataifa ya Haki za binadamu inatumika nyakati za amani, na sheria zote mbili zinakutana katika nukta moja muhimu nayo ni kumlinda binadamu na haki zake, na tofauti iliyopo kati ya sheria mbili hizi ni kwamba Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inalenga kuwalinda raia wa adui katika nyakati za vita, wakati Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu imejikita katika kumlinda mtu mmoja mmoja dhidi ya ukandamizaji ambao huenda ukafanywa na nchi ya raia huyo.
Kutokana na mgawanyo huu, tunaweza kuifasili Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu kuwa ni mjumuisho wa vifungu vya kisheria vyenye lengo ya kumlinda binadamu na haki zake katika nyakati za migogoro ya kutumia silaha.

Na kwa kukumbushia yale ambayo yalishatajwa hapo nyuma, kwamba Uislamu unaviangazia vita kuwa ni dharura ambayo inapimwa kwa hitajio lake, pia na kutokana na fasili iliyotangulia kuhusu Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu, tunaweza kugundua mambo mawili muhimu katika sheria hii, nayo ni kwamba, kwanza vita vinapasa kuwepo kwa kiasi cha dharura tu kwa kiasi na namna, na pili ni kwamba yote yatakayojiri wakati wa vita au dharura hii yanatakiwa yawe ni yenye kulinda na kuheshimu ubinadamu.

Mambo mawili haya ni miongoni mwa misingi ya Sheria ya Kiislamu. Msingi wa kwanza ni ule ujulikanao kama (Dharura) huu unaelezwa katika Sheria ya Kiislamu kwamba dharura hukisiwa ufumbuzi wake kwa kiasi ilivyo dharura yenyewe, na madamu vita ni dharura basi haifai kwa hali yoyote ile kufanya jambo la ziada nje ya dharura hii, na uvukaji wowote wa mpaka wa dharura hii utahesabika kama ni uadui dhidi ya mtu mwingine.

Ama msingi wa pili, huu hujulikana kama (Ubinadamu), ni kwamba kimsingi binadamu ametukuzwa na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anasema ***"Na hakika tumewatukuza wanaadamu…" (17:70)*** na pia Mwenyezi Mungu amekataza dhulma akasema ***"…Na atakaye dhulumu miongoni mwenu tutamwonjesha adhabu kubwa." (25:19)*** na hili ni onyo kwa kila mwenye kudhulumu, yeyote yule ikiwa ni pamoja na mtu kumdhulumu mtu mwingine nyakati za vita. Na kwa mujibu wa kanuni hii Uislamu umewataka wafuasi wake kuingia vitani huku wakiwa wamejipamba na roho ya ubinadamu, kwamba haifai kwa muislamu kuingia vitani isipokuwa kwa sababu za kisheria ***"Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini." (6:151)*** na pindi itakapopatikana hasa sababu ya kisheria, hapo itapasa kupigana kwa njia za kibinadamu zilizo bora zaidi, ikiwa ni kuifanyia kazi Hadithi iliyopokewa na Shadad bin Aus (Mwenyezi Mungu amridhie) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema *"Hakika Mwenyezi Mungu ameandika wema katika kila kitu, hivyo basi, mkiua ueni vizuri na mkichinja mchinje vizuri".* (Sunan At-Tirmidhi)

Na Mtume (juu yake rehema na amani) amefupiliza namna ya kuoanisha kati ya hali ya vita na hali ya kushikamana na kanuni mbili hizi aliposema *"Mimi ni Mtume wa huruma pia ni Mtume wa vita"* (Ibn Sa'ad) hapa ameviambatanisha vitu viwili ambavyo ni vita na huruma, ila ametanguliza huruma kabla ya vita ili kumfundisha muislamu kuwa yeye ni msingi wa uadilifu na si mtu

wa mambo mabaya na ukatili, ni kwamba, inapotokea hali ya dharura ya vita hatakiwi kusahau tabia nzuri na huruma.

Tunapozungumzia suala zima la tabia nzuri katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu kwamba inachukua nafasi kubwa katika mtazamo na utekelezaji wa Sheria ya Kiislamu (kama ilivyoelezwa hapo juu) basi yale matukio ya hali ya kipekee ambayo mtu anashindwa kuidhibiti nafsi yake kwa sababu moja ama nyingine ya mazingira ya vita ambapo humpelekea kusahau maadili na tabia zake nzuri, matukio haya yana mtazamo wa kipekee katika Sheria ya Kiislamu.

Kwa mara nyingine, Uislamu unatumia tena njia nyingine ya kusisitiza umuhimu wa kushikamana na tabia njema kwa kuwataka wafuasi wake kudhibiti hisia zao mbaya. Na ndipo tunaona kuna maandiko mengi ya kisheria yanasifu na kukumbusha juu ya umuhimu wa kushikamana na tabia njema, kwa mfano:

1. Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu ***“Ambao hutoa wanapo kuwa na wasaa na wanapo kuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema” (3:134)*** hapa amesifiwa yule mwenye kuidhibiti nafsi yake baada ya kuchukia, ni yule aliyezuia hasira zake na kusamehe.

2. Amesema Mwenyezi Mungu ***“Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanao subiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.” (41:34-35)*** Hapa kuna ukumbusho juu ya kushikamana na tabia nzuri na kumtendea wema adui, na jambo hili si kila mtu analiweza, hili lina watu wake ambao wenye sifa za uvumilivu na subira, hawa ni wale watu wenye hadhi kubwa.

3. Kutoka kwa Abu Huraira (Mwenyezi Mungu amridhie) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema *“Shujaa si yule mwenye kuwashinda watu kwa kupigana (kama vile kupigana mieleka) bali shujaa ni yule anayeweza kuizuia nafsi yake pindi akishikwa na hasira”.* (Al-Bukhari na Muslim)

   Hivyo basi, kuizuia nafsi wakati hakuna lolote na katika hali za kawaida si kitu kikubwa, kazi ngumu ni kuizuia nafsi wakati wa hasira.

4. Na Mtume (juu yake rehema na amani) anasema *"Mwenye kuzuia hasira, hali ya kuwa anaweza kuipitisha (kwa kufanya lolote), mtu huyo ataitwa na Mwenyezi Mungu mtukufu siku ya Kiyama mbele ya kadamnasi ya watu na atampa hiari ya kuchagua idadi atakayo ya wanawake wazuri-huur-een".* (Sunan Abu Dawud)

Hasira si mazingira ya kawaida, lakini Uislamu umepambana na hali hii kwa kukumbushia tabia nzuri na kusifu nafasi kubwa ya mwenye kujipamba na subira, mtu ambaye hajakubali kuwa mateka wa hisia zake zenye kumpeleka kwenye tabia mbaya zisizopendwa.

Uislamu umethamini na kusisitiza sana juu ya tabia njema na kuahidi malipo mazuri ya duniani na akhera kwa lengo la kuhamasisha zaidi kushikamana nazo kwa watu wote, viongozi na wasiokuwa viongozi. Hii ni kwa ajili ya kuifanya tabia njema kuwa ndio kipimo muhimu, kwamba, watu kila wanaposhikamana na tabia njema ndipo wanapokuwa hawana haja ya sheria ambazo kimsingi ni lazima zifuatwe, na kinyume chake ni hivyo hivyo, kwamba tabia njema zinapolegalega huwa kuna ulazima wa kutunga sheria ngumu ambazo zitapelekea kuweka hali ya amani duniani, ila sheria hizi mara nyingi huwa zinavunjwa, na kwa kuwa mfumo wa kikomunisti ni mfumo usioamini Mwenyezi Mungu, badala yake unaamini maadili na tabia nzuri, imewajibika kwao kutunga sheria hizi na kuzitekeleza, lakini pamoja na hayo sheria hizi hazijaweza bado kufanya kitu chochote ukilinganisha na mchango mkubwa unaotolewa na malezi ya tabia nzuri kuhusiana na kuwalinda binadamu.

Na tukitafuta sababu ya Uislamu kusisitizia sana tabia nzuri katika mambo mengi tutagundua kwamba upande wa tabia nzuri ndio upande pekee unaofaa kwa kuyafanya mambo yatengamae.

Kwani tabia nzuri zinapopatikana ndipo haki za binadamu zinapolindwa katika nyakati za vita na amani na hapo ndipo watu huishi katika amani.

Kufuatia hayo yaliyotangulia imebainika kwamba Uislamu umethamini nafasi ya tabia nzuri katika hali ya kawaida ambayo ni hali ya amani, pia umethamini sana nafasi ya tabia hiyo katika hali za kipekee yakiwemo mazingira ya vita, hayo yote ni kwa ajili tu ya kulinda haki za binadamu ambazo mara nyingi huwa zinakiukwa katika vita. Na hapa ndipo inapoonekana kwa nini Uislamu umejikita zaidi katika kulea na kukuza tabia nzuri kwa watu katika mazingira yote. Na kila nafsi ya binadamu inapokutana na hali ngumu ndipo Uislamu nao

kwa upande wake huwa unaikumbusha nafsi hiyo juu ya kuwa na tabia nzuri na maadili mema, yote haya ni kwa lengo la kumtaka binadamu amheshimu binadamu mwenzie katika hali ya hasira na furaha, awe ni adui au rafiki.

Huu ndio msingi mkuu ambao Uislamu umeuweka kwa wafuasi wake kwa ajili ya kumlinda binadamu dhidi ya binadamu mwingine hasa katika nyakati za hatari zaidi, nyakati za vita ambazo huwa zimegubikwa na mazingira ya dhulma na uadui. Na hili ndilo linatoa taswira ya ujumla ya muelekeo wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu inayolenga kuimarisha tabia nzuri na maadili, kwa namna ambayo ni ya kipekee kabisa.

## PEKUZI YA KWANZA

# SEHEMU ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

# SEHEMU ZA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

Uislamu ni dini ya amani, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu…" (2:208)***. Uislamu umeweka tahadhari mbalimbali ili kuzuia na kuepuka vita, na endapo itatokea dharura ya waislamu kuingia vitani basi Uislamu pia umeweka misingi na sheria za kupunguza madhara ya vita hivyo, kwamba madhara hayo yaishie kwa wapiganaji wenyewe tu na yasiwafikie wananchi wengine ambao hawahusiki na vita, pia Uislamu umeweka sheria ya kuwalinda mateka dhidi ya madhara ya vita hata baada ya kuisha kwa vita hivyo.

Na ili kutoa dodoso tu juu ya misingi hii tutaweka hapa baadhi ya haki ambazo Uislamu umeziweka ili kuwalinda wahanga wa vita na migogoro ya kutumia silaha, nazo ni kama ifutavyo:

## 1. KULINDA HAKI ZA MAJERUHI NA WALIOKUMBWA NA MAJANGA

Pindi majeruhi wa upande wa adui anaposhindwa kubeba silaha na kupambana na waislamu, hapo ni lazima aachwe pasi na kushambuliwa au kufanyiwa ubaya wowote, na zaidi ya hapo, ni lazima kumlinda na kuishi nae vizuri mhanga huyu. Huu ni utekelezaji wa msingi muhimu wa sheria isemayo, vita ni dharura, na dharura hukisiwa ufumbuzi wake kwa kiasi ilivyo dharura yenyewe. Kwa mujibu wa msingi huu, dharura hii inapoisha tu, papo hapo vita inabidi iishe, vivyo hivyo mwanajeshi anapokuwa hawezi tena kupigana huwa haifai kuuawa au kumdhuru kwa chochote, sambamba na hayo, pia haifai kumtesa majeruhi, kwa sababu kufanya hivyo hakusaidii chochote kwenye vita, ni kwamba majeruhi anapokuwa ameshindwa kabisa kupambana inatakiwa azingatiwe kuwa ni mateka wa vita, na wala si vinginevyo, hii ni kwa sababu ya kuheshimu utu wake, na kwa kuzingatia kwamba lengo la vita ni kuidhoofisha nguvu ya adui, hivyo haifai kuvuka mpaka huo na kufanya uadui zaidi. Anaeleza Abu Ubeid Al-Qaasim bin Salaam katika kitabu chake Al-Amwaal (Kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) alimwamrisha

mtangazaji wake siku ya kuifungua Makka awatangazie watu kuwa, *"Chonde chonde asiuliwe Majeruhi, wala asifuatwe mwenye kukimbia, na wala asiuliwe mateka, na mwenye kufunga mlango wake basi huyo amesalimika"*. Wahba Al-Zuheily naye kwa upande wake anasema: 'Tangazo hili haliwahusu watu wa Makka tu peke yao, hili ni tamko kwa wote, na inatakiwa lieleweke hivyo hivyo kwa upana wake kama lilivyo'.

Hivyo basi waislamu wakishapata uhakika kwamba sasa wameshinda, watatakiwa haraka sana wakae vizuri na mateka, kwani Uislamu ni dini ya huruma kwa wote, na mtu anapokuwa ni majeruhi au mgonjwa huwa anahitaji huruma zaidi.

Vile vile majeruhi ana haki ya kupata matibabu ya jeraha lake, kwa kuzingatia kwamba maandiko yanayowataka waislamu kuwafanyia wema mateka yanahusisha pia kuwatibu majeruhi hawa. Imam At-Twabraniy anaeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) anasema *"wausieni heri mateka"* hii ni pamoja na kuwatendea muamala mzuri ambao kwa ujumla wake ni pamoja na kuwapatia matibabu, na kinyume chake, kukosa kuwapatia matibabu stahiki ni sawa na kuwatesa, jambo ambalo limekatazwa na Sheria ya Kiislamu, anasema Mwenyezi Mungu mtukufu, ***"...wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui." (2:190)*** Na imekuja katika Hadithi iliyopokewa na Hisham bin Hakiim bin Hizaam, amesema nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akisema: *"Hakika Mwenyezi Mungu atawaadhibu siku ya Qiyama wale ambao wanawatesa watu duniani"* (Sahihi Muslim) Na jambo la kuwatesa watu linapingana na misingi mizuri pamoja na tabia njema ambazo Uislamu unafanya juu chini kuwafundisha wafuasi wake.

## 2. HAKI ZA MATEKA

Mateka wa vita wanaokusudiwa hapa ni wale maadui ambao waliufanyia uadui Uislamu nje nje kisha pakazuka vita na wao wakaangukia chini ya mikono ya Waislamu.

Kihistoria, hapajawahi kutokea mpiganaji ambae alikaa vizuri na maadui zake kama walivyoishi waislamu wa mwanzo na maadui zao, waislamu ambao walifuata maelekezo ya dini yao, ikiwa ni pamoja na kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu, ***"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu.***

***Hatutaki kwenu malipo wala shukrani." (76:8-9)***

Na Uislamu umempa mateka umuhimu wa kipekee, umuhimu ambao unaheshimu hadhi yake na kulinda haki zake pamoja na kuzuia dhulma yoyote dhidi ya haki hizo. Na maelezo yafuatayoni mjumuisho wa baadhi ya mambo yanayohusiana na namna ya kuishi na mateka katika Uislamu:

1. Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu katika Surat Al-Anfaal ***"Ewe Nabii! Waambie mateka waliomo mikononi mwenu: Kama Mwenyezi akiona kheri yoyote nyoyoni mwenu atakupeni bora kuliko vilivyo chukuliwa kwenu, na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu." (8:70)*** tunachojifunza hapa ni kwamba, kwa kuwa Mwenyezi Mungu mtukufu anawaahidi msamaha mateka ambao nyoyo zao ni safi, hivyo ni wajibu wa waislamu kuishi nao vizuri zaidi kwa huruma na ubinadamu.

2. Uislamu umewataka waislamu kuishi vizuri na mateka na umekataza kuwadharau au kuwadhalilisha na kuutweza utu wao. Ameeleza At-Twabaraniy kupitia hadithi aliyoipokea Abii Aziz kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema *"Wausieni heri mateka"* (At-Twabaraniy) Na katika vita vya Bani Quraydhah ambapo Mayahudi walitengua ahadi iliyopo kati yao na Mtume (juu yake rehema na amani) kwamba hawafai kuwaunga mkono washirikina dhidi ya waislamu, walipofanya uhaini huu na kutengua ahadi hii, jambo ambalo lilipelekea kuhatarisha maisha ya waislamu, Mtume (juu yake rehema amani) aliwazingira kisha akawaweka kizuizini. Kwa upande mwingine, waislamu walipohakikisha kwamba wameshawashinda na kwamba Mayahudi wamekuwa ni mateka chini ya Mtume, Mtume huyo huyo aliwaambia maswahaba zake *"kaeni vizuri na hawa mateka, muwaache walale usingizi wa mchana, na muwape vinywaji mpaka watosheke"*. Na kwa upande wake naye Imam Malik (Mwenyezi Mungu amrehemu) alipoulizwa kwamba, 'Je inafaa mateka kuteswa endapo kutakuwa na matumaini kwamba kwa kufanya hivyo atataja madhaifu ya adui?' Alijibu: Sijawahi kusikia kitu kama hicho' Kauli hii ina mazingatio yake na katika masuala haya kuna rai nyinginezo.

3. Kutokana na ukarimu wake, Uislamu umewataka waislamu kuwalisha mateka, ikiwa ni kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu mtukufu. Bali Mwenyezi Mungu ameielezea tabia ya kuwalisha mateka kuwa ni sifa ya watu wema ambao wana nafasi za juu kabisa kati ya waislamu, kwani

anasema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa." (76:8)*** maana ya aya hii ni kwamba, wanawalisha chakula hao waliotajwa hapo juu ilhali waislamu wenyewe wanakipenda chakula hicho kwa sababu ya njaa waliyokuwa nayo, na licha ya hali hiyo, wameanza kuwatanguliza hawa wasiojiweza, ambao ni maskini, yatima na mateka. Kinachokusudiwa hapa sio kuwalisha tu peke yake, bali ni kuwafanyia wema kwa maana pana zaidi, hapa kimetajwa chakula kwa kuwa ndio wema mkubwa zaidi, na hapa ndio panapodhihiri vipi mtu anamtanguliza mwenzake katika jambo zuri, na kwa kawaida huwa si rahisi mtu kumpatia mwenzake chakula ilhali yeye mwenyewe ana njaa na anakihitaji chakula hicho, na ikitokea hivyo basi ni kwa kuwa yule mtu alikuwa na tabia nzuri sana, hivyo basi, si ajabu kuwaona maswahaba wa Mtume (juu yake rehema na amani) walikuwa wakiwalisha mateka wao vyakula vizuri zaidi kuliko ambavyo walivyokuwa wanakula wao wenyewe majumbani mwao. Anatuelezea Abu Aziz bin Umeir ambaye alikuwa ni mmoja wa mateka kwamba (Maanswaar waliporudi kutoka vita vya Badri, nilikuwa (mateka) katika kundi lao, basi walipokuwa wakileta chakula cha mchana au usiku walinipa mimi peke yangu mikate na wao wenyewe wakala tende, walikifanya hivyo ili kutekeleza wosia wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) basi ilikuwa mtu akiwa na kipande cha mkate ananipatia mimi kwanza, nami nilikuwa naona haya nikakataa na kumpa mtu mwingine ambaye naye pia alikataa na kunirudishia mimi tena.

Anasema Abu Yusuf (Mwenyezi Mungu amrehemu) (hakuna budi kumfanyia wema mateka wa washirikina mpaka ahukumiwe). Na si katika wema kumuacha mateka bila chakula au mavazi yanayomkaa sawa sawa. Na viongozi wa Kiislamu walishikamana na mwenendo huu katika vita vyao, walikuwa wanawakirimu mateka, hawawaachi na njaa kabisa, na historia imeelezea msimamo huu ulioonekana pia kwa Salaah Diin Al-Ayubiy (Mwenyezi Mungu amrehemu) alipokuwa anapigana vita vya msalaba. Itakumbukwa kwamba aliteka idadi kubwa ya jeshi la Wafaransa, lakini kwa kuwa alikuwa hana chakula kinachowatosha hawa aliamua kuwaachia huru, ila sasa walipoungana na kuunda jeshi dhidi yake, alipongeza jambo hilo na kuona kuwa ni bora awaue katika viwanja vya mapambano kama wapiganaji lakini si kuwaua kwa njaa wakiwa ni mateka chini yake.

4. Na katika muamala mzuri wa kuishi na mateka ni kumpa mavazi ambayo yataendana naye, yatakayomlinda na joto kali pamoja na baridi, kwani

Jabir (Mwenyezi Mungu amridhie) amepokea hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) kwamba siku ya Vita vya Badri walileltwa mateka mbali mbali akiwemo  Abbas ambaye alikuwa hana nguo, basi Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akatafutatafuta akapata nguo ya Abdallah bin Yaqdir, akamvalisha. Na kuna habari kadhaa kwamba Mtume alitoa baadhi ya nguo zake na kuwapa mateka.

5. Na katika haki za mateka ambazo Uislamu umeziweka kwa mateka ni pamoja na kumruhusu kutekeleza ibada zake kwa kipindi chote ambacho atakuwa ni mateka. Ni vema ikafahamika kwamba Uislamu humruhusu mateka kufanya ibada zake, hiyo ni zaidi ya uhuru wa mtu kutoingiliwa katika imani yake au kumlazimisha kuingia katika Uislamu, anasema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu…" (2:256)***.

6. Uislamu haumfanyii hiana mateka na hata kama itatokezea adui kufanya hivyo yaani kutokutekeleza ahadi waliowekeana na waislamu na kufanya hiana basi waislamu hawatakiwi kufanya hivyo kutokana na kauli ya Mwenyezi mungu mtukufu, ***"Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine" (35:18)*** na kulingana na hadithi ambayo imetupitia hapo nyuma, kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) alituma jeshi lake na kuwaambia, "*Tokeni kwa jina la Allah, piganeni na waliomkufuru Mwenyezi mungu, msivunje ahadi wala msizidishe, wala msimithilishe (kumkatakata maiti) na msiue watoto wala watu waliopo sehemu za ibada*" (musnad Al-Imam Ahmad). Imekuja katika kitabu cha historia ya mitume na wafalme cha Ibn Jariir At-Tabari kuwa khalifa wa Umawy Mu'awiya bin Abi Sufyaan ambae alilazimika kuweka mkataba wa amani pamoja na warumi na kuchukua kutoka kwao rehani kama dhamana ambayo ilitumika kama watawadanganya, hata hivyo wakadanganya na kwenda kinyume na ahadi yao, pamoja na hayo walirejeshewa rehani yao na kuambiwa: "Kwa hakika mkabala wa udanganyifu huo na kutotekelezwa ahadi ni bora kuliko mkabala wa udanganyifu kwa udanganyifu."

7. Na miongoni mwa njia za kuishi vizuri na mateka ni kutowatenganisha mateka wa familia moja, imepokewa hadithi kutoka kwa Abi Ayoub amesema kuwa amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu -juu yake rehema na amani- akisema ( Mwenye kumtenganisha mama na mtoto wake, Mwenyezi Mungu atamtenganisha yeye na wapenzi wake siku ya Kiyama) Imam Tirmidhiy anasema na ili kuyafanyia kazi maneno haya,

wamekubaliana wanazuoni wote kuanzia kwa maswahaba wa Mtume (juu yake rehema na amani) mpaka wanazuoni wa sasa kuwa haifai kuwatenganisha mama na mtoto wake au kati ya baba na mwanawe au ndugu zake. Naye Imam Bin Qudaamah anasema katika kitabu chanke Al-Mughniy 'Wanazuoni wamekubaliana kuwa haifai kuwatenganisha kati ya mama na mtoto wake' namna hiyo hiyo haifai kuwatenganisha kati ya baba na mtoto wake, wala kati ya ndugu wawili wa kike au wa kiume, bali kuna baadhi ya wanazuoni wameenda mbali zaidi na kusema kuwa haifai kuwatenganisha ndugu wa familia moja kama vile shangazi na mtoto wa kaka yake na mama mdogo pamoja na dada yake. itakumbukwa kwamba Kiongozi wa Kiislamu enzi za utawala wa Dola ya Abbaasiyah ajulikanaye kwa jina la Al-Motasim Billaah alizivamia na kuziteka ngome za Armenia baada ya vita vikubwa sana, ila aliamrisha kwamba pasitenganishwe kati ya mateka wa wana familia moja.

8. Uislamu umewazuia wanajeshi wake kufanya vitendo vya mihemko vyenye misukumo ya kihisia, hivyo umezuia mtekaji kumuua mateka wake, awe ni mtu mmoja au kundi, ni kwa sababu inawezekana yule mateka akamkosea au alimkosea mwanajeshi wa kiislamu ambaye naye kwa upande wake ataitumia fursa hii kulipiza kisasi, jambo ambalo halifai kulingana na mtazamo wa kiislamu, na ndiyo maana pakawekwa sheria kwamba wanajeshi wote wasubiri nini ataamua Amiri jeshi Mkuu pale atakapokuwa ametulia. Kufanya hivi huwa kunaepusha kufanya maamuzi ya hasira na kunampa mateka heshima na utu wake. Na hili ndilo ambalo fiqhi yake imetulia kwa wanazuoni kuwa jambo la mateka lipelekwe kwa hakimu ambapo ataona ambalo ni bora zaidi kufanywa. Anasema Bin Qudaamah, 'Na mwenye kupata mateka haifai kumuua, bali amlete kwa Imam ambaye ataangalia amfanye nini, kwa sababu mtu anapokuwa ni mateka hapo jambo lake linakuwa chini ya imam' katazo hili linamlinda mateka na sura za ghadhabu ya adui na furaha yake yenye kupitiliza ya ushindi ambayo inawapata wanajeshi wakati wa utekaji, na wakati huo mara nyingi hutokea mauaji dhidi ya mtu na dhidi ya haki ya wanajeshi wanaposhindwa na kuangukia katika mikono ya wanajeshi wa upande wa pili.

Na kwa kuzingatia katazo hili, mwanajeshi yeyote atakuwa hawezi kumfanyia uadui mateka wa mwanajeshi mwingine, hivyo hata akimuona mwanajeshi mwenzake yupo na mateka hatafikiria kwenda kumuua. Ushahidi wa hili ni hadithi iliyopokewa na Samura (Mwenyezi Mungu

amridhie), kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema *'Imekatazwa kabisa, mmoja wenu kuvamia mateka wa mwenzake kisha amchukue na kumuua'.*

**9.** Uislamu mara zote umekuwa ni wenye kumuonea huruma mateka, na ndiyo maana kumuacha huru mateka kunahesabika kuwa ni miongoni mwa tabia njema ambazo Waarabu wamejisifia nazo, anasema mtunga mashairi:

*'Na hatuui mateka bali tunawaacha huru pindi shingo zinaposhindwa kutoa gharama za fidia'*

Na aya inayojulikana zaidi kuhusu hukumu ya mateka ni neno lake Mwenyezi Mungu mtukufu,

***"Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe…" (47:4)*** Hivyo hukumu ya mateka punde tu atakapotiwa mbaroni ni kuwahifadhi mpaka vita viishe, kisha hakimu wa kiislamu atakuwa na hiari ya kutoa hukumu yoyote kati ya hizi zifuatazo:

**Mosi:** Kumsamehe na kumuacha huru pasi na malipo yoyote. Hukumu hii Mtume (juu yake rehema na amani) ameifanya sana baada ya vita tofauti alivyoshiriki, kama ambavyo imeandikwa katika vitabu vya historia yake, na hili si jambo la kushangaza kwa sababu hata Mwenyezi Mungu mwenyewe ameanza na msamaha ***"…Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe…" (47:4)*** na kutenda wema maana yake ni kusamehe na kumuacha huru mateka pasi na malipo yoyote. Kwamba umetangulizwa msamaha kabla ya hukumu nyingine, hapa kuna maana kubwa sana, na ndiyo maana Mtume (juu yake rehema na amani) baada ya Vita vya Badri aliichagua hukumu hii kwanza kabla ya hukumu nyingine. Mtume (juu yake rehema na amani) alisema siku ya Vita vya Badri lau kama Mut-am bin Adiy (ambaye alikuwa ni kigogo wa wanaopinga Uislamu) angelikuwa hai na akawaombea mateka wa Badri waachwe huru, ningewaacha huru kwa ajili yake. Yote haya yanaonesha ni kiasi gani Sheria ya Kiislamu imethamini kuwasamehe mateka.

**Pili:** Ama chaguo la pili ni Kutoa fidia. Inawezekana mateka akatoa kiasi fulani cha mali kama fidia ya kuikomboa nafsi yake, kama ilivyotokea katika vita vya Badri, au mateka wa kiislamu aliyeko chini ya wasiokuwa waislamu atolewe fidia, na Mtume hakuishia hapo tu katika kuwaachia huru mateka kwa kutoa mali tu peke yake, bali aliwataka wale mateka wanaojua kusoma wawafundishe kusoma na kuandika watoto wa kiislamu, mateka akitekeleza hilo anaachwa huru, na hili ni jambo ambalo lipo ndani ya uwezo wa mateka na ni jepesi kwake, pia hili linaakisi utashi wa dini ya kiislamu katika kuwapa watu uhuru na kupiga vita ujinga.

**Tatu:** Chaguo la tatu ni mateka kuuawa. Wenye mtazamo huu wana ushahidi wao kutoka katika Qur'an na Hadithi, ni pamoja na yaliyotajwa katika vitabu vya historia ya Mtume kwamba aliamrisha mateka kuuawa. Ibin al Arabi (Allah amrehemu) amenukuu kauli ya Ibin Abbaas (Mwenyezi Mungu amridhie) akisema ***"mpaka awe ameshinda baraabara katika nchi" (8 :67)*** na hii ilikuwa ni siku ya Vita vya Badri wakati waislamu walikuwa ni wachache, ama ilipozidi idadi ya waislamu na kuwa ni wengi Allah alisema, ***"...Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe..." (47:4)*** hapo ikawa ni hiari ya kuchagua moja ya mambo mawili tu na hii ndio kauli ya wanazuoni wengi, kati ya kuwasamehe na kuwaacha huru bila malipo au kuwaacha huru kwa njia ya kutoa fidia, na hii ni kauli ya baadhi ya wanazuoni wa Sheria ya Kiislamu ambao wamekataza kumuua mateka. Bin Rushdi baada ya kunukuu tofauti za wanazuoni kuhusiana na kadhia hii alisema: 'Na wanazuoni wengi wanaona kwamba Imam ana hiari ya kumsamehe mateka' kumfanya awe mtumwa au kumuua, kisha akasema 'Na kuna wanazuoni wanasema kuwa haifai kumuua mateka'. Kwa upande wake naye Al-Hassan bin Muhammad Al-Tamimiy anasema kuwa haya ndiyo makubaliano ya maswahaba wa Mtume na hata Imam Hass na 'Atwai nao wanasema kuwa 'Haifai kwa Imam kumuua mateka' na anasema Abu Hayyan katika kitabu chake Al-Bahr Al-Muhiitw wakati akiitafsiri kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu ***"Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe...." (47:4)*** anasema 'ni dhahiri kwamba kukata shingo au kuua kwa kuwafunga kamba -wakati wa mapambano, na kwamba kauli yake ima muwasamehe baada ya kuwafunga kamba au watoe fidia- kwamba kuna hali mbili kwa mateka, ima asamehewe, kama Mtume (juu yake rehema na amani) alivyomsamehe Thamama bin Athali Al-Hanafiy, au atolewe fidia, kama ambavyo Mtume aliruhusu kubadilishana mateka, hivyo mateka wawili wa

wasiokuwa waislamu walitolewa fidia kwa mateka mmoja wa waislamu, na hukumu hii inapingana kabisa na mtazamo wa kuua. Lengo la vita katika Uislamu sio kummaliza adui bali ni kuzuia uadui wake, hivyo basi uadui ukishadhibitiwa, na baadhi ya wanajeshi wakishakuwa ni mateka ilhali hawana makosa yoyote ya kivita au makosa yoyote makubwa, hapo huwa haifai kuwaua.

**10.** Hapo nyuma tulielezea kuwa desturi inazingatiwa kuwa ni msingi wa kisheria katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu, hivyo basi nchi zikishasaini mikataba au kuwa na desturi kwamba ni lazima kumlinda mateka asiuliwe baada ya kutekwa, mkataba au desturi hii itakuwa ni lazima itekelezwe kwa upande wa Dola ya Kiislamu, na sehemu hii ya desturi itakuwa ni wajibu kutekelezwa na wote, ikiwa inatokana na sehemu ya Sheria ya Umma ya Kimataifa iliyojengwa juu ya mikataba au desturi ambayo itakuwa ni wajibu kutekeleza hivyo hata kama itaonekana kuwa ule uamuzi wa hakimu utakuwa umebanwa, kwa sababu katika kufanya hivyo kuna masilahi kwa pande zote mbili, na dola ya Kiislamu inajali sana kulitekeleza hilo, ama mashirikiano kati ya jumuiya ya kimataifa katika kutekeleza mikataba na desturi hii itakuwa ni moja kati ya njia za kumlinda mateka na kumpa heshima na utu wake.

## 3. HAKI ZA WATU WALIOPOTEA NA MAITI

Baada ya vita watu wengi hupotea pasi na kupatikana taarifa zao zozote, jambo hili huwa linatia simanzi na majonzi makubwa, na uchungu huu huwa ni mkali zaidi kuliko hata kusikia habari ya kifo chenyewe, ni kwa sababu machungu haya huwa hayana mwisho, na hupelekea ndugu kutamani kujua kama ndugu zao wamefariki au laa ili warejee katika hali zao za kawaida.

Hivyo basi, imekuwa ni lazima kwa waislamu kutoa taarifa kwa upande wa adui kuhusiana na mateka waliokuwa nao, na haipendezi kuficha majina ya mateka au kukanusha uwepo wao chini ya waislamu, kwani kufanya hivyo ni kumtia unyonge mateka na kupoteza haki zake za kisheria ikiwa ni pamoja na kuheshimu utu wake na kuwapa ndugu zake maelezo yenye kujitosheleza kuhusu ndugu yao.

Ni muhimu sana kupata taarifa za mwanajeshi baada ya kila vita, pamoja na kukusanya habari za kila mwanajeshi hasimu aliyepotea au kufariki vitani na mwili wake kubaki kwa waislamu, ni kwa sababu Uislamu umemtukuza

binadamu katika hali zote mbili, akiwa hai au amefariki. Yafuatayo ni baadhi ya maelekezo kuhusu kumtukuza binadamu baada ya kufariki katika nukta hizi zifuatazo:

1. Mtume (juu yake rehema na amani) amekataza kukatakata mwili baada ya kufa. Bureida amepokea hadithi akisema; 'Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu pindi anapomteua mtu kuwa Mkuu wa Majeshi au Kikosi, akimuusia kheri, katika yale ambayo huwa anaiusia nafsi yake na anayowausia waislamu walio pamoja naye, kisha huwa anasema: *"Piganeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, katika njia ya Mwenyezi Mungu, mpigeni mwenye kumpinga Mwenyezi Mungu. Piganeni vita, wala msiibe mali, msikatekate maiti, wala msiue mtoto mdogo.* (Sahihi Muslim) Na imepokewa hadithi kutoka kwa Anas bin Malik (Mwenyezi Mungu amridhie) amesema kuwa 'Haijawahi kutokea Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) atoe hotuba kisha asiamrishe kutoa sadaka na kukataza kukatakata maiti'. (As-Sunan Al-Kubra, Al-Baihaqi)

   Ikumbukwe, katika vita vya Uhudi wakati maadui walikatakata maiti za waislamu, Mtume (juu yake rehema na amani) (kama ilivyonukuliwa katika tafsiri At-Tabariy) alisema, 'endapo tutawashinda, tutakatakata maiti zao thelathini', waislamu waliposikia hivyo walisema, Wallahi tukiwashinda tutawakatakata kwa namna ambayo waarabu hawajawahi kufanya hivyo kwa yeyote, pale pale likashuka neno la Mwenyezi Mungu mtukufu, ***"Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri." (16:126)***

   Anasema Imam Twabriy: Mtume pale pale akabadili maamuzi na kutangaza kwamba miili isikatwekatwe tena, na akakataza kufanya hivyo. Kwa msingi huu, haifai kukatakata mwili wa adui. Amesema Imam As-Swan'aaniy katika kitabu chake Subul salaam kuwa Hadithi ya Bureydah iliyotangulia hapo juu inaharamisha kukatakata maiti na kuua watoto wa wasiokuwa waislamu, kisha akasema 'Na haya ni makubaliano ya wanazuoni wote'. Az-Zamakhshariy naye kwa upande wake anasema, 'Hakuna tofauti yoyote kati ya wanazuoni kwamba haifai kukatakata maiti, na kuna hadithi nyingi za kukataza hilo bali nyingine zimekataza hata kukatakata mbwa mwenye kung'ata watu hovyo, sembuse binadamu.

**2.** Uislamu umekataza kubeba vichwa vya maiti na kuvitembeza. Anasema Imam Az-Zuhriy "Haijawahi kutokea kabisa, kichwa kubebwa na kupelekwa kwa Mtume (juu yake rehema na amani)" (Al-Baihaqiy). Na amepokea Muhamad bin Hassan Ash-Shaibaniy kwamba Uqba bin 'Amir Al-Jahni alibeba kichwa cha maiti fulani hivi ambaye hakuwa ni muislamu na kukipeleka kwa Kiongozi wa Waislamu Abu Bakar (Mwenyezi Mungu amridhie) Abu Bakar akakataza tabia hiyo na papo hapo akawaandikia makamanda wake kwamba:

'Sitaki kuletewa vichwa, na mkifanya hivyo mtakuwa mumevuka mipaka, mimi natosheka kwa kuletewa taarifa tu na habari sahihi'. Na inasemekana alisema: 'Haya mambo ya kubebabeba vichwa haya ni mambo ya waajemi'. Hii inamaanisha kwamba kubeba vichwa si katika muongozo wa Sheria ya Kiislamu tangu mwanzoni mwa Uislamu, kama ambavyo kauli ya Abu Bakar kwamba 'haya mambo ya kubebabeba vichwa haya ni mambo ya waajemi' inaonesha wazi kuikosoa tabia hii, ikimaanisha kwamba jambo hilo halifai, na ingelithibiti kwamba kuna ushahidi wa kutokea hilo basi ingelikuwa ni kwa wale tu maadui waliovuka mipaka, kama ambavyo historia inavyotuonesha katika mifano inayotajwa katika vitabu vya historia kuhusaina na wale watu ambao vichwa vyao vilibebwa baada ya vita. Hivyo basi, hukumu hii inakuwa ni finyu mno ikiwahusu maadui maalum waliovuka mipaka na kuwafanyia waislamu maudhi makubwa sana.

**3.** Ili kulinda utu wa binadamu, haifai kuacha maiti wazi ziliwe na wanyama au kudonolewa na ndege, bali maiti inatakiwa ifukiwe na kulindwa dhidi ya vitendo ambavyo vitazingatiwa kuwa ni dharau, kwa maana, kama ambavyo Uislamu umekataza kukatakata maiti pia umeamrisha kulinda miili hii isitafunwetafunwe au kudonolewa na ndege wakubwa. Kuna hadithi zinazoelezea kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) alifukia mizoga ya wasiokuwa waislamu, kwani katika Vita vya Badri Mtume (juu yake rehema na amani) aliamrisha kwamba miili yote ya wasiokuwa waislamu ivutwe na kutiwa katika shimo, kama ambavyo alifukia mwili wa Umayah bin Khalaf ambapo walishindwa kuufikisha kule kisimani. Inaonekana hapa kwamba Mtume hakuiacha miili hii iliwe na wanyama, na ilikuwa ni tabia ya Mtume (juu yake rehema na amani) kwamba akipita katika maiti yoyote ile ataamrisha ifukiwe pasi na kutaka kujua kwamba maiti hiyo ni ya muislamu au laa, imepokewa Hadith kutoka kwa Ya'ala bin Murah amesema,'Mimi nimesafiri na Mtume (juu yake

rehema na amani) zaidi ya mara moja, kwa hakika, sijawahi kumuona akipita mbele ya maiti ya mtu yeyote kisha aivuke tu hivi hivi (kama hajaona kitu) bali alikuwa anaamrisha izikwe, tena wala haulizi kamwe kama ni muislamu au sio muislamu.'

Kutokana na mjumuisho wa maandiko yaliyotangulia tunaweza kusema kuwa Uislamu umewajibishakuzika maiti za adui, ni kwa kuzingatia tu ubinadamu wao, kisha Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa wanachostahili. Huku ndiko kumtukuza binadamu kwa vitendo, awe yuko hai au ni maiti, pasi na ubaguzi wowote wa kidini au imani.

## 4. HAKI ZA RAIA

Sheria ya Kiislamu imetambua kanuni inayotaka kutofautisha kati ya wapiganaji na raia wa kawaida tangu karne kumi na nne zilizopita, kama ambavyo imetambua ulazima wa kutofautisha kati ya kambi za jeshi na vyanzo vya huduma za kijamii. Kwani maandiko ya kisheria ndani ya Uislamu na utekelezaji wa kivitendo vimeonesha ni kiasi gani inatakiwa kutofautisha kati ya raia na wapiganaji kwa upande mmoja, na baina ya kambi za jeshi na vyanzo vya huduma za kijamii kwa upande mwingine, sambamba na hayo, Sheria ya Kiislamu imeamuru kuwalinda raia na kutowadhuru, Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu ***"Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui." (2:190)***

Ibin Al-Arabiy (Mwenyezi Mungu amrehemu) ameitafsiri aya hii akisema 'Ni wapiganaji tu wanaofaa kupigwa vita, nao ni wanamume waliobaleghe. Ama wanawake, watoto na viongozi wa dini hao haifai kuuawa'. Na Ibin Abbas naye ametafsiri kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu ***'Wala msivuke mipaka'*** kwamba, 'Msiue wanawake, watoto na wazee' ijulikane kuwa, vipofu, viongozi wa dini, wakulima na wengineo hao wote wanaingia katika kundi hili.

Na kwa msisitizo zaidi, Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) alikuwa akiwausia wanajeshi wake pindi anapowatuma kwenda kupigana vita na maadui juu ya kutofautisha kati ya wapiganaji na raia wa kawaida, imepokewa hadithi kutoka kwa Anas bin Malik (Mwenyezi Mungu amridhie) amesema, Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema, *"Nendeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa kufuata mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, msiuwe*

*mzee mwenye kutoweka, wala mtoto mdogo au mwanamke, wala msifiche mali, na kusanyeni ngawira zenu, na mkafanye vizuri hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kufanya vizuri"* (Abu Dawud)

Katika wosia huu tunaweza kuona kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa akisisitiza kwamba haifai kuwaua watu wa aina tatu, nao ni:

**a.** Mzee kikongwe
**b.** Mtoto mdogo
**c.** Mwanamke

Na alikuwa akisema mara kwa mara *"Msiue mzee kikongwe wala mtoto wala mwanamke"*

Ni kwa sababu mafungu haya matatu kawaida huwa hayashiriki vita, na kwa kuwa lengo la vita katika Uislamu si kumuua adui bali ni kuzuia uadui wake, hivyo imekuwa haifai kuvuka lengo hili la vita. Na kwa muktadhaa huu haifai kuwauwa watu wote ambao hawashiriki katika vita kwa namna moja ama nyingine, kwani hao watahesabika kuwa ni raia wa kawaida wanaoingia katika ile ile sababu kuu ya kuwa hawashiriki vita.

Na wosia huu umejirudiarudia katika maelekezo mengi ya Mtume (juu yake rehema na amani) kwa makamanda wake wa jeshi ambao walikuwa wanatoka kwenda vitani mara kwa mara, kwani alikuwa akiwaamrisha daima kwamba wasiue wanawake, watoto na watu wa masinagogi. Miongoni mwa maelekezo hayo ni pamoja na kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) katika Hadithi iliyopokewa na Ibin Abbas (Mwenyezi Mungu amridhie) kuwa Mtume pindi alipotuma majeshi yake alikuwa akisema *"Tokeni kwa jina la Mwenyezi Mungu mtukufu, mkapigane vita na anayempinga Mwenyezi Mungu, msivunje ahadi wala msizidishe wala msiibe mali, msikatekate maiti wala msiue watoto na watu wa masinagogi"* na Hadithi nyingine iliyopokewa na Ka'ab bin Malik kutoka kwa Ami yake, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani ziwe juu yake) pale alipotuma jeshi kwenda kwa Ibin Abi Al-Huqaiq katika mji wa Khaibari alikataza kuua wanawake na watoto) na imepokewa hadithi kutoka kwa Ibin Umar (Mwenyezi Mungu amridhie yeye na baba yake) ameeleza kwamba, katika moja ya vita alivyoshiriki Mtume (juu yake rehema na amani) palipatikana mwanamke ameuawa, Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akakataza kuua wanawake na watoto.

Na imam Ahmad ameipokea Hadithi kwamba Mtume alisema: *"Huyu mwanamke alikuwa hapigani vita"*, kisha akakataza kuua wanawake na watoto wadogo.

Na huu ni ufafanuzi wa sababu ya kukataza kuua wanawake nayo ni kwamba kukosa kupigana vita, hivyo basi, asiyepigana vita si halali kumuua.
Na Mtume (juu yake rehema na amani) alimuusia Khalid bin Al-Walid akimwambia, *"Usiue kizazi wala mfanyakazi"*.

Maelekezo yote yaliyotangulia hapo juu yanasisitiza kwamba haifai kuwagusa wananchi wa kawaida kama vile wanamke, watoto wadogo, wazee na mfano wa hao, miongoni mwa watu ambao hawashiriki kupigana vita.

Pia katika Hadithi zilizopita kuna Hadithi moja imeongeza kundi jipya la watu ambao halifai kuuawa nao ni watu wa masinagogi, nao ni wale watawa ambao wanatumia muda wao mwingi kufanya ibada makanisani au katika sehemu zao za kuabudu. Kiongozi wa Kiislamu Abu Bakar aliandika wosia uliosomeka kwamba 'wala msivunje sehemu za ibada za wasiokuwa waislamu'. Katika wosia huu tunaweza kuelewa mambo mawili, kwanza ni kwamba Uislamu unaheshimu viongozi wa dini na watawa, na kwamba linakataza kuwafanyia ubaya wowote, wao na wengineo wanaofanana nao ambao hawashiriki katika vita. Jambo la pili ni kwamba ikiwa haifai kuwagusa wafanya ibada basi sehemu zao za ibada ndio haifai kabisa kuzikaribia kwa kipindi chote cha vita, kwa sharti kwamba sehemu hizi zisitumike kwa shughuli za kijeshi. Na kwa muono wangu (mtunzi wa kitabu hiki) ni kwamba, hukumu hii inakusanya pia sehemu za tamaduni kama vile maktaba na shule pamoja na vyuo vikuu na mfano wake, kwa sababu sehemu hizi hazina tofauti na sehemu za ibada kiutendaji, malengo na watu wanaokusanyika humo.

Na Abu Bakar (Mwenyezi Mungu amridhie) alifanyia kazi maelekezo haya, kwani alipomteua Yazid bin Abu Sufyan (Mwenyezi Mungu amridhie yeye na baba yake) kuwa ni Kamanda mkuu wa jeshi alilolituma kwenda miji ya Sham, alimuusia kwamba asiue wanawake, watoto wadogo, na watawa, isipokuwa kama watawakwaza waislamu kutekeleza majukumu yao. Na pia ilisomeka sehemu ya wosia kuwa '*na mtakutana na watu wamejifungia katika masinagogi yao, hao waacheni na mambo yao*' na inajulikana kwamba kipindi hicho miji ya Sham ilikuwa imejaa masinagogi ya mayahudi na mahekalu ya watawa na sehemu tofauti za ibada ambazo walikuwa wanatekeleza sala zao humo, hivyo wosia huu wa Abu Bakar ulikuwa na manufaa makubwa, ni kwa sababu hawa

walikuwa hawana mahusiano yoyote na vita, iwe kimtazamo au utekelezaji. Hivyo basi, haifai kuua watawa na watu wa masinagogi. Na hata Ibin Katheer nae ameeleza hivi hivi katika kitabu chake cha tafsiri ya Qur'an.

Ikumbukwe kwamba katika wosia wa Abu Bakar kwa Yaziid bin Abi Sufyaan kuna maelezo yalisomeka pia *'wala msiue mtoto mdogo, mwanamke, mzee kikongwe, mgonjwa wala mtawa, na wala msikate mti, msiharibu jengo, na wala msichinje ngamia au ng'ombe isipokuwa kwa ajili ya kula tu, wala msizamishe mtende wala msiuchome moto'.*

Hapa tunajifunza kuwa wasia wa Abu Bakar (Allah Amridhie) umejumuisha katazo la kukata mti wa matunda, kuharibu jengo kumchinja mnyama mwenye kuliwa pasopo na lengo la kumla, vivyo hivyo kuuzamisha mitende.

Wosia uliotangulia hapo juu umevitilia msisitizo vitu ambavyo leo hii tunaweza kuviita kuwa ni vyanzo vya huduma za kijamii au kuharibu mali za adui bila kuvitumia.

Wanazuoni wa kiislamu wametofautiana ikiwa inafaa au haifai kuharibu mali za adui ambazo hazikutumika vitani. Mwanachuoni Ibin Qudamah ameigawanya miti na mazao katika makundi matatu:

**Kundi la kwanza:** miti ambayo adui ameifanya kuwa ndio ngome ya kujikinga nayo au anaitumia kwa matumizi ya kijeshi ambayo endapo yatabakia yatamnufaisha adui. Miti hii inafaa kukatwa kwa makubaliano ya wanazuoni wote. Ni kwa sababu huwa inatumika kwa shughuli za kivita.

**Kundi lapili:** Ni miti ambayo kubaki kwake kunawanufaisha waislamu, na haijazoeleka miti hiyo kukatwa. Miti hii haifai kukatwa.

**Kundi la tatu:** Ni miti ambayo haipo katika makundi hayo mawili yaliyotangulia, ambayo hakuna faida yoyote itakayopatatikana endapo itakatwa labda ni kwa lengo tu la kuwakera maadui peke yake, kundi hili lina kauli mbili za wanazuoni. Kauli ya kwanza imezigawanya mali za adui katika makundi mawili, nayo ni vitu na wanyama, kauli hii imeweka wazi kuwa inafaa vitu kuharibiwa lakini si wanyama. Ama kauli ya pili imesema kwamba inafaa kuharibu mali za adui zisizotumika katika vita kwa ajili ya kumdhoofisha na kumkera.

Kimsingi, mgawanyo huu unarudi katika sheria ile ile ya kutofautisha kati ya raia na mpiganaji, na kati ya kambi ya jeshi na vyanzo vya huduma za kijamii. Hivi huoni katika wosia wa Abu Bakar kuna katazo la kukata miti yenye matunda, kuharibu jengo, kuzamisha mtende au kuchoma? Hivyo basi, haifai katika Sheria ya Kiislamu kuelekeza mashambulizi yoyote kwa raia au kuwaua, vivyo hivyo, haifai (kwa mtazamo wa jamhuri ya wanazuoni) kuharibu vyanzo vya huduma za kijamii, kama ambavyo ameeleza Ibin Qudamah hapo juu, na yeyote atakayeenda kinyume na haya, huyo atakuwa ameingia katika kundi la waliovuka mipaka wasiopendwa na Mwenyezi Mungu, anasema Mwenyezi Mungu ***"Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msipetuke mipaka. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui."*** (2:190). Na kwa hakika kukata miti hovyo na kuua wanyama pasi na hitajio ni uvukaji wa mipaka, na si uadilifu, hali ya kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha waumini kuwa waadilifu akasema, ***"Sema: Mola Mlezi wangu ameamrisha uadilifu..." (7:29)***.

Hivyo si katika uadilifu kuelekeza mashambulizi ya kijeshi dhidi ya raia.

Ijulikane kuwa, haifai kumshambulia raia hata kama si muislamu, kwani jambo la imani ya mtu na malipo yake, hayo ni kati yake yeye na Mwenyezi Mungu siku ya Kiama.

Lengo la kupigana vita ni kumzuia na kuzuia fitna za mpiganaji, na asiyepigana hahusiki na hilo, nao ni lile kundi la wazee, watawa, wanawake, watoto wadogo na mfano wao, hao hawahusiki na lengo la vita.

Hivyo basi kila mwenye uwezo wa kupigana vita ikiwa hajashiriki vita hivyo haifai kumshambulia, kwa sababu licha ya kwamba katazo limewajumuisha watawa na wanawake, hali ya kuwa miongoni mwao wapo ambao wana uwezo wa kupigana ila kwa kuwa walijiweka mbali na mapigano na hawakuchangia kwa rai au kuunga mkono, wamehesabika kuwa ni miongoni mwa raia wa kawaida ambao uislamu unalinda haki zao katika nyakati za vita. Hivyo, haifai kwa kamanda wa jeshi la Kiislamu apambane nao.

Na katazo hili linakusanya pia sehemu za ibada, vituo vya tamaduni, shule na mfano wa hayo. Na utekelezaji wa haya umeonekana katika vita vya maswahaba walipoifungua miji ya Sham, kwani kwa hakika, waliyaacha makanisa na watu wake, ambapo waislamu hawakufanya ubaya wowote dhidi yao, si wakati wa mapambano kati ya pande mbili au baada ya mapambano.

## PEKUZI YA PILI

# UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU

### (TUTATUMIA MFANO WETU WA VITA VYA BADRI)

# PEKUZI YA PILI

# UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU YA KIISLAMU (VITA VYA BADRI NI MFANO TOSHA)

Ni rahisi kutunga sheria na kuweka mfumo ambao utalenga kuweka usawa na uadilifu wakati wa amani na vita, ila ni vigumu kutekeleza sheria hizo kivitendo, ikiwa ni pamoja na kuyafanya madhumuni yaliyomo katika sheria hizo kuwa ni tabia elekezi hasa katika suala zima la vita. Kwani mara nyingi na kwa haraka sana sheria hizo nzuri husahaulika wakati wa vita ambapo sheria ya misituni huchukua nafasi yake, wakati huo ole wake aliyeshindwa kwa ubabe wa mshindi atakavyofanya.

Kutokana na hayo, nimeona nisiishie kuandika mambo ya nadharia tu peke yake, bali pia nitaje baadhi ya mifano ya utekelezaji wa kivitendo wa yaliyoelezwa hapo nyuma kuhusu Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu, ni kwa kueleza uhalisia wa vita vikali ambavyo waislamu walikutana na maadui zao ambapo baada ya makabiliano mazito kati ya pande mbili hasimu waislamu walishinda vita hivyo.

Baada ya vita hivi vikali hebu tujiulize !! Kuna uhalisia gani wa nadharia tuliyoijadili hapo nyuma katika viwanja vya vita?
Ni swali ninalouliza na jibu lake naliacha kwenye tukio lililokwishatokea, ni mfano halisi ambapo Mtume (juu yake rehema na amani) alitekeleza ubinaadamu na utu ndani ya vita hivyo.

Jibu hili huelezea kiwango cha utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu, kwa maana, kuonesha haki za binadamau ambazo Mtume (juu yake rehema na amani) amezitekeleza kivitendo katika vita vya Badri.

Lakini kabla hatujaanza kuelezea Vita vya Badri na yaliyojiri ndani yake, ngoja kwanza tujiulize swali: Ni kwa nini nimechagua Vita vya Badri?

1. Ni kwa sababu hivyo vilikuwa ndivyo vita vya kwanza vya kupambana uso kwa uso kati ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) na Maqureish wasiokuwa waislamu, hivyo basi, huu ulikuwa ndio mtihani wa kwanza wa kivitendo wa utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu, pia ulikuwa ndio utekelezaji wa kwanza wa kivitendo baada ya kuishi muda mrefu kinadharia tu.

2. Ni kwa kuwa vita hivi vilizuka baada ya uadui mkubwa sana kati ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) na baada ya maudhi na kero nyingi kutoka kwa Maqureishi wasiokuwa waislamu dhidi ya Mtume na maswahaba zake, hivyo basi, kwa kawaida, hapa watu walitaraji kwamba jeshi la waislamu lingelipa kisasi kwa kiasi kikubwa sana, kwa kuzingatia kwamba kabla ya hapo walikuwa wakidhulumiwa, kuonewa na kupokonywa haki zao.

3. Kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliwashinda watesi wake wazi wazi kabisa.

4. Kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa na idadi kubwa ya mateka baada ya vita.

Na labda picha itakuwa wazi zaidi baada ya kuilezea vita hii kama ifuatavyo:
Muhamad (juu yake rehema na amani) alipewa utume katika mji wa Makka, akawa anawalingania watu wamuamini Mwenyezi Mungu mtukufu, pia alikuwa akiwakataza watu kumshirikisha Allah, na kwamba wanatakiwa wakae mbali na mambo machafu yanayochukiza, na wajiepushe na tabia mbaya, hapo alipambana na maudhi na changamoto nyingi kutoka kwa vigogo wa Maqureishi yakiwemo maudhi ya kila aina pamoja na ya kimwili, si hivyo tu, bali hata wale walioitika wito wa Uislamu waliadhibiwa na kuteswa sana kiasi kwamba baadhi yao walifariki dunia, jambo ambalo liliwafanya baadhi yao kuhamia Uhabeshi (Ethiopia) wakitafuta uhuru wa kuabudu huku wakiwa na amani. Na kutokana na kuendelea kwa mfululizo wa kero na maudhi haya kundi jingine la pili likahama kutoka Makka kwenda uhabeshi.

Maudhi yalipoendelea kwa Mtume (juu yake rehema na amani) pamoja na wafuasi wake Mtume aliwapa ruhusa wafuasi wake kuhamia mji wa Madina,

ambapo baadaye yeye Mwenyewe na wafuasi wake wengine walihamia huko pia, wakiwa wameacha kila walichokuwa nacho vikiwemo mali na ardhi zao ambazo wale wasiokuwa waislamu walizipora na kuzihodhi.

Cha kushangaza ni kwamba, baada ya wale wasiokuwa waislamu kusikia kwamba Mtume na wafuasi wake wanahama, walimfuatilia kwa lengo la kumdhuru, bali walitangaza zawadi nono kwa yeyote atakayefanikiwa kumleta akiwa hai au amekufa. Na hata walipojua kwamba amefika salama salmini katika mji wa Madina hawakumuacha hivi hivi, bali walimpinga sana hadi kuzuka matambiano ya kijeshi kati ya pande mbili hizi, yaliyopelekea kuzuka kwa vita vya Badri. Hapo ni baada ya miaka miwili tangu kuhama kwake.

Vita vya Badri vilitokea katikati ya njia baina ya Makka na Madina. Idadi ya wasiokuwa waislamu ilikuwa ni watu elfu moja (1000), wakati idadi ya waislamu ilikuwa ni mia tatu na kumi na nne tu (314), ambapo wasiokuwa waislamu walishindwa, na kati ya hao watu sabini waliuawa na watu wengine sabini walitekwa.

## MAZINGATIO YA KIBINADAMU YALIYOPATIKANA KATIKA VITA VYA BADRI

Baada ya muhutasari huu juu ya Vita vya Badri, kuna mazingatio mawili makubwa ambayo yanawakilisha mazingatio mengine yaliyobaki ya kibinaadamu, nayo ni :

1. Mazingatio yanayohusu namna Mtume (juu yake rehema na amani) alivyoishi na wanajeshi wake
2. Namna ambayo Mtume (juu yake rehema na amani) alivyoishi na mateka.

Tutaelezea mazingatio haya pasi na mengine ili kumpa muhtasari ndugu msomaji, kwani kwa kutumia mifano hii lengo litakamilika na ndugu msomaji atafananisha mazingatio yaliyobaki kwa kutumia mifano hii.

### Mosi: Mazingatio ya kibinadamu yanayohusu namna Mtume (juu yake rehema na amani) alivyoishi na wanajeshi wake:

1. Mtume (juu yake rehema na amani) aliishi na jeshi lake kana kwamba na yeye ni mmoja kati ya wanajeshi hao, kwani ilikuwa huwezi kumtofautisha yeye na wengine, na katika vita hivi kuna ushahidi wa kivitendo juu ya hilo. Ni kwamba, jeshi la Mtume lilitoka likiwa na watu mia tatu na kumi

na kitu hivi, pia kulikuwa na farasi wawili pamoja na ngamia sabini ambao wale wanajeshi walikuwa wakipokezana kupanda, mara anapanda huyu na mara nyingine anapanda huyu, ni kwa sababu walikuwa na wanyama wachache wa kuwapanda. Kwa upande wao, Mtume (juu yake rehema na amani) na Ally bin Abi Twalib pamoja na Marthad bin Abi Murthad Alghanawiy walikuwa wakipokezana kupanda ngamia mmoja, na hata pale walipomwambia Mtume (juu yake rehema na amani) kwamba aendelee kupanda yeye tu, aliwajibu kuwa *"Msidhani kwamba ninyi mna nguvu kuliko mimi, wala msidhani kuwa mimi nimetosheka na thawabu kuliko nyinyi".* (Al-Mustadrak) Ikumbukwe kwamba, wakati huo, Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa na umri wa miaka hamsini na tano, na umri wa Ally bin Abi Twalib ni miaka ishirini na tano, na licha ya hivyo, waliendelea kupokezana kupanda ngamia mmoja.

Kwa kiongozi, msingi wake wa kuheshimu haki za binadamu unaanzia pale anapojishusha kwa wanajeshi wake, na kinyume chake, pale kiongozi anapokiuka haki za binadamu na kujihisi kuwa yeye ni mkubwa zaidi ya wanajeshi waliomzunguka, ambapo huanza kumdhulumu huyu na kuvunja heshima ya yule, athari ya tabia hii huwa ni kwamba mwanajeshi aliyeshuhudia haya akipata fursa ya kuwa na mateka kutoka kwa jeshi hasimu atalipiza kisasi.

Kiongozi anapojishusha, msingi wa kuheshimu haki za binadamu nao unaimarika, na kiongozi ambae anaamiliana na askari wake katika hali hii ndiye ambae anaweza kupandikiza hisia za kumuheshimu binadamu, heshima hii hudhihiri pale anapomkamata mateka wa upande wa adui katika viwanja vya vita.

**2.** Katika Vita vya Badri ulidhihiri pia msingi wa Mashauriano na Kuheshimu mtazamo au rai ya mtu mwingine, kwani inajulikana kuwa Mtume alikuwa akiwaambia maswahaba zake *'Enyi watu haya naomba rai zenu'* baada ya hapo kundi la Muhaajirina (waliohama kutoka Makka kwenda Madina) na wengineo kutoka kabila la Aus na Khazraji walitoa maoni yao tofauti, kama ambavyo Habbab bin Al-Mundhir na wengineo wengi walizungumza. Pia katika vita hii Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa akibadili mbinu zake kadhaa za kijeshi kulingana na mitazamo ya wanajeshi wake na ushauri wao. Hapo alikuwa akiwafundisha na kuwaonesha wale aliokuwa nao kwamba ni kiasi gani anawaheshimu watu na kuupa utu thamani yake, pia alikuwa akiwafundisha kwamba mtu asimdharau mwingine, bali

anatakiwa atambue kwamba kila mtu ana mchango wake, ima kwa sababu ya nguvu zake za kiwiliwili au akili yake. Jambo hili ni vigumu sana kuliona kwa viongozi wa jeshi wa sasa.

Kiuhalisia, viongozi na makamanda wa jeshi huwa hawatoi fursa ya majadiliano hata kwa viongozi waliokuwa nao, achilia mbali kwamba maongezi haya yataheshimiwa au laa. Lakini Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa akisikiliza na akitaka ushauri pamoja na kuheshimu mitazamo, bali alikubali mpaka kubadilisha mbinu alizopanga, jambo hili lilikuwa likimfanya yule mzungumzaji aone kwamba rai yake imeheshimiwa na kusilikizwa bali na kutekelezwa pia, kwani uhuru wa kutoa maoni hauishii katika kuweza kuzungumza tu, bali ni kumpata mtu atakayeweza kusikiliza rai yako, kuiheshimu na kuifanyia kazi. Hivyo basi, kuwa na jeshi ambalo limelelewa katika mazingira haya, na kushikamana na misingi ya kuheshimu rai ya mtu mwingine, na kuheshimu mitazamo, jeshi hili ni lazima litaheshimu haki za watu wengine, wala halitaweza kukiuka misingi iliyotajwa hapo juu, hata kama litapigana vita na adui ambae anatofautiana nao kimtazamo.

3. Katika Vita vya Badri, tena wakati wa kunyoosha safu ziwe sawa sawa, tunaweza kujifunza kitu kingine ambacho kitatuwekea wazi ni kiasi gani Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa na pupa ya kuwaridhisha wanajeshi wake, na namna gani alikuwa anataka uadilifu uwepo na haki isimame walau ni ya mtu mmoja tu, ni pale alipomruhusu mmoja wa wanajeshi kumlipiza kisasi yeye mwenyewe; ni kwamba, Mtume (juu yake rehema na amani) alipita karibu na Sawad bin Ghaziya (Mwenyezi Mungu amridhie) na Sawad alikuwa yuko nje kidogo ya safu, Mtume akamkandamiza Sawad kwa fimbo yake na kumwambia: ‘Simama sawa sawa ewe Sawad, Sawad akasema, Yalaa! Umeniumiza ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ilhali Mola amekuleta kutenda haki, hivyo hakuna budi nami nikulipize kisasi (akimaanisha kwamba na wewe Mtume usimame hapa ili nikulipize) basi Mtume (juu yake rehema na amani) akafunua tumbo lake na kusema: ‘Haya njoo ulipize, papo hapo Sawad akamkumbatia na kumbusu. Mtume (juu yake rehema na amani) akamuuliza: Enhe! Nini kilichokufanya utende hivi ewe Sawad? naye akajibu: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, unaona hali ilivyo hapa, (akimaanisha kwamba kumekuwa ni sehemu ya kufa shahidi) hivyo nimependa uwe mwisho wangu wa kuonana na wewe ni kwamba ngozi yangu iguse ngozi yako, basi Mtume naye (juu yake rehema na amani) akamuombea kheri’

Hivyo basi, ikiwa Amiri Jeshi mkuu anaweza kupokea malalamiko ya ajabu kutoka kwa mmoja wa wanajeshi wake, na anamruhusu kulipiza kisasi, haiwezekani siku moja aje kukiuka au kukandamiza haki yoyote ya binadamu, iwe ni kwa wanajeshi wake au kwa maadui zake. Na kwa upande mwingine, huyu mwanajeshi anayeshuhudia heshima hii kutoka kwa kiongozi wake, anayeshuhudia uadilifu wa kivitendo kutoka kwa Mkuu wake, pia naye haiwezekani siku moja aje kukiuka haki pale atakapokuwa amemshinda adui yake.

## Pili: Mazingatio ya kibinadamu juu ya namna Mtume alivyoishi na mateka

**a.** Mtume alifanikiwa kuteka watu sabini (70) katika vita hivi, watu hawa hawakuwa ni mateka tu, bali pia walikuwa ni wahalifu wa kivita kama inavyotamkwa hivi sasa, kwani walikuwa na makosa mengi yanayohusiana na kumuudhi Mtume (juu yake rehema na amani) ikiwa ni pamoja na jaribio la kutaka kumuua na kumtoa katika mji wake na kuwaadhibu maswahaba zake wengi, kiasi kwamba baadhi yao walifariki dunia wakiwa katika mateso, ni kwa sababu tu waliamua kumfuata Mtume (juu yake rehema na amani). Mtume alipoweza kuwadhibiti hakuwaua watu wote sabini, bali waliuawa watu wawili tu kati yao, na ni kwa sababu maalumu zinazohusiana na mateka hawa kwa mambo waliyoyafanya hapo nyuma kabla ya vita

**b.** Mtume alikaa vizuri na mateka pia alipowakabidhi kwa maswahaba zake aliwausia kwamba (wakae nao vizuri). Wosia wa Mtume (juu yake rehema na amani) ni kanuni inayowahusu mateka wote. Na bila shaka wosia huu ulikusanya mambo yote mazuri yanayohusu makazi, chakula na kukaa vizuri na mateka. Kukosa kutekeleza jambo moja katika haya yaliyotangulia ni kuupunguza wosia wa Mtume wa kukaa vizuri na mateka wa Mtume, na Mtume alikua akiwagawanya mateka kwa maswahaba zake ili maswahaba waweze kuwahudumia vizuri mateka. Imam Baidhwawiy anasema katika kitabu chake cha tafsiri ya Qur'an : Ilikuwa hivi, 'Mtume analetewa mateka naye humkabidhisha mateka huyo kwa baadhi ya waislamu huku akisema kaa naye vizuri'.
Na hii inamaanisha kwamba mateka hawa walikuwa wakiishi katika nyumba za maswahaba au walikuwa wakiishi msikitini.

Historia imeandika ushahidi mwingi kutoka kwa mateka hawa, ifuatayo ni baadhi ya mifano:

**Mosi:** Anasema Abu Aziz bin Umeir ambaye alikuwa ni mmoja wa mateka, nilikuwa mmoja wa mateka wa vita vya Badri chini ya kundi la Maanswari, basi walikuwa wakileta chakula chao cha mchana au usiku mimi wananipa mkate (kwa kuwa kilikuwa chakula kizuri zaidi), na wao walikuwa wakila tende tu, walifanya hivyo ili kutekeleza wosia wa Mtume (juu yake rehema na amani) uliowataka kukaa vizuri na sisi mateka, na ilifikia kwamba mtu yeyote akipata kipande cha mkate hunipa mimi kwanza, jambo hili lilinafanya nione haya nikamrudishia yule mtu mkate wake, naye pia hunirudishia mimi wala hachukui mkate huo.

**Pili:** Anasema Abu Al-Asi bin Rabiy mmoja wa mateka (nilikuwa katika kundi la Maanswar, Mungu awalipe kila la kheri, tukawa tukila chakula cha usiku au mchana wao hunitanguliza mimi kula mkate na wao wakala tende, ilifika kwamba mtu akipata kipande cha mkate mkononi mwake hali bali hunipa mimi.

**Tatu:** Walid bin Walid bin Mugheera anasema mfano wa hayo hayo na anazidisha kwamba na wao Maanswar walikuwa wakitupakiza sisi vipando vyao, ilhali wao wakitembea. Anamaanisha kwamba mateka alikuwa akipanda farasi au ngamia na swahaba anatembea kwa miguu.

Mazingatio yapatikanayo kutokana na ushahidi huu wa mateka ni kwamba maswahaba walikuwa wakiwatanguliza mateka kwa kuwapa chakula kizuri, na hii inamaanisha kwamba maswahaba hawakuwa sawasawa na mateka katika chakula bali mateka walikuwa wakipatiwa chakula kilicho bora zaidi huku maswahaba wakila chakula kilicho chini ya viwango. Pia mateka walikuwa wakipanda wakati maswahaba walikuwa wakitembea kwa miguu.

Hili hawezi kuliamini asomae historia ya vita vya kale na vya sasa. Tunaona wakati ule na wa sasa vile vile namna gani haki zinavyokiukwa kwa sababu ndogo sana na damu zinavyomwagwa na heshima za watu na utu wao unapoondolewa

Kama hali ndivyo zilivyo basi si ajabu na kumkosa mtu ambae atawapa chakula kizuri mateka na kumtanguliza kuliko hata nafsi yake na kumpa kipando na yeye kukikosa.

**d.** Mwanazuoni Abdu Razak anaeleza katika kitabu chake kisa kimoja cha huruma dhidi ya mateka akisema (Abbas alipotekwa siku ya Vita vya Badri, alikuwa amefungwa kamba kisawasawa hivyo akawa anaugulia, Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) alimsikia akashindwa kulala kabisa usiku ule. Mtu mmoja katika Maanswar akagundua hilo, basi akasema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hakika unakesha usiku kucha, Mtume naye akajibu Abbas ananifanya nikeshe, kamba zimempa maumivu makali, hilo ndilo linalonikosesha usingizi, yule mtu akasema kwa nini nisiende kumlegezea kamba kidogo? Mtume akajibu: Kama itakupendeza kufanya hivyo kwa niaba yangu. Yule Answariy akaenda kwa Abbas akailegeza ile kamba na Abbas akatulia tuli, basi hapo Mtume (juu yake rehema na amani) akapata usingizi. Hivi ndivyo ambavyo Amiri Jeshi Mkuu alikua makini na mateka wake. Nani leo hii anaewafikiria mateka na hali zao, na inaeleweka kwamba mateka wenyewe huwekwa kambini na wanajeshi wa kawaida tu na si amiri jeshi mkuu!

**e.** Miongoni mwa namna ya kukaa vizuri na mateka tunayoweza kuisoma katika vita hivi, ni huruma yake Mtume kwa mabinti wa mateka na upole wake, kwani Mtume alimuacha huru mateka mmoja bila ya kuchukua chochote kwake, kwa sababu ya kuwahurumia binti wa mateka huyu. Amepokea Imam Waqidi kutoka kwa Said bin Musayyib amesema: Siku ya Vita vya Badri Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na Amani juu yake alimdhamini Abu Azza Amri bin Abdallah bin Umeir Al-Jumhi (ambaye alikuwa ni msanii mzuri wa kutunga mashairi) akamwacha huru, jambo hili lilitokea pale Amri alipomwambia Mtume (juu yake rehema na amani) kuwa mimi nina mabinti watano na hawana chochote, hivi unaonaje ewe Muhammad ukinitolea sadaka na kunitendea wema? Mtume akafanya hivyo.

**f.** Suheil bin Amri alikuwa ni mmoja kati ya viongozi wa Maqureishi, alipojua kwamba Mtume wa mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) ametoka ili kuhodhi mali na msafara wa Maqureishi aliwahamasisha watoke wakapambane na Mtume (juu yake rehema na amani) na yalipokutana majeshi mawili katika Vita vya Badr Amri alikuwa ni mmoja wa mateka, Umar bin Khatwab (Mungu amridhie) akasema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu niruhusu nimtoe meno yake asiweze kusimama tena na kufanya kampeni mbaya dhidi yako, Mtume (juu yake rehema na amani) akasema: 'Siwezi kumfanyia hivyo na Allah akanifanyia mimi hata kama mimi ni nabii, na huenda akafika sehemu ambayo wewe hutoichukia'.

Nani leo hii katika viongozi wa vita anaeweza kusema haya! Kwa kawaida, Hakika jambo la kwanza analolifanya kiongozi punde tu baada ya kushinda vita ni kulipa visasi, haswa kwa wale ambao walikuwa wakifanya kampeni dhidi yake, lakini Mtume (juu yake rehema na amani) anatuonesha kwa vitendo kwamba, mtu hata kama atakuwa na uadui kiasi gani atabaki kuwa ni binadamu tu mwenye haki zake zote, na haifai kuvuka mipaka ya ubinadamu, hivyo haifai kuudhiana wala kutesana bali kama ilivyopita huko nyuma ni kuheshimu nafasi ya binadamu na hata kama ikiwa mtu huyu ni miongoni mwa viongozi wa maadui waliofanya kampeni dhidi ya waislamu kabla ya kuwa mateka.

Kutokana na muongozo huu wa kumtukuza binadamu tunaona wanazuoni wa sheria ya kiislamu wamezuia kumtesa adui au kumkatakata, anasema Az-Zamakhshary (Hakuna tofauti yoyote kati ya wanazuoni kuhusiana na kuharamisha kumkatakata maiti, bali zimepokewa hadithi nyingi zinazokataza kufanya hivyo hata kwa mbwa anaeng'ata).

**g.** Mtume (juu yake rehema na amani) si kwamba aliwatilia umuhimu mateka kwa vitu vya lazima vya mahitaji ya kibinadamu tu, bali pia alitilia umuhimu mpaka mavazi ya mateka. Imepokewa hadithi katika Sahihi Bukhari kutoka kwa Jabiri (Mungu amridhie) amesema, '*Vilipozuka Vita vya Badri alileta Abbas akiwa hana nguo, basi Mtume akamtafutia kanzu ya Abdullah bin Abi Al-Harith ndio iliyokuwa inamfaa na akamvalisha. Kama ilivyopokewa vile vile kuwa Mtume aliwavalisha baadhi ya mateka kanzu zake*''. (Sahihi Al-Bukhari)

Imam Wakidi naye anaeleza tukio lingine la kuishi vizuri na mateka kuwa Khalid bin Hisham bin Mugheera aliingia yeye pamoja na Umaiyya bin Abi Hudhaifa bin Mugheera (na hawa wawili walikuwa ni mateka) walifika nyumbani kwa Ummu Salama (Mungu amridhie) (pia walikuwa ni ndugu wa Ummu Salama) basi Ummu Salama aliposikia habari zao alitoka na kuanza kumtafuta Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) kisha akamkuta kwa Bi Aisha (Mungu amridhie) akamwambia, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa hakika watoto wa ammi zangu wameomba waingie nyumbani kwangu, wawe ni wageni wangu niwapokee vizuri na kuwakirimu, na kuwapaka mafuta nywele zao na kuwatuliza ila sikupenda kufanya hivyo bila ya kuomba ruhusa yako, naye Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akasema mimi sichukii chochote katika hayo fanya upendavyo.

Ni ajabu kabisa ukarimu huu kwa mateka ambao umefikia kuwageuza mateka kuwa ni kama wageni, ambao watapakwa nywele zao mafuta na kutulizwa, je, kuna namna gani nyingine ya kuishi vizuri na mateka inayofanana na hii !?

**h.** Picha nyingine mpya kabisa ya kuishi vizuri na mateka tunaipata baada ya Mtume (juu yake rehema na amani) kufika mji wa Madina akiambatana na mateka. Hakika alizingatia uwezo wa kila mateka, kwamba kama kulikuwa na mateka fukara, huyo alimuacha pasi na kuchukua chochote kutoka kwake, na kuna wengine aliwaacha huru kwa sababu ya kusilimu kwa mzazi wao, kwa mfano Wahab bin Umeir Al-Jumhi ambaye aliachwa huru kwa kuthamini kusilimu kwa baba yake.

Ametaja bin Kathiir (Mungu amrehemu) kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliwaacha huru mateka kadhaa pasi na kuchukua chochote kutoka kwao, kama vile Abu Al-Asi bin Rabii Al-Umawiy, Al-Mutwalib bin Hantab na Swayfiy bin Abi Rifaa. Pia kuna wale ambao walikuwa wanajua kusoma na kuandika, fidia yao ilikuwa ni kwamba kila mateka awafundishe watoto kumi wa kiislamu kusoma na kuandika. Na hii inaonesha ni kiasi gani Uislamu unamuheshimu mateka na kumtukuza, kwani licha ya kwamba mtu huyu ni mateka ila bado atabaki kuwa ni mwalimu mwenye heshima zake. Na kwa upande mwingine jambo hili linaonesha ni kiasi gani Uislamu unaitukuza elimu na kuwa na pupa ya kuieneza kati ya waislamu.

Lakini kwa upande wa wale mateka waliokuwa wanajiweza, hawa walitoa fidia, pia tunaona kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) alipokea fidia ya mali hata kwa Ami yake Al ‘Abbas ambaye alikuwa ni mmoja wa mateka, tena huyu alitoa fidia kubwa zaidi kuliko hata mateka wengine, hii ni kwa sababu ya kuondosha dhana ya upendeleo kwa ami yake, ikumbukwe kwamba wale waliomteka Abbas walimuomba Mtume (juu yake rehema na amani) amuachie huru bila malipo yoyote, lakini Mtume (juu yake rehema na amani) alikataa na kuamrisha kwamba asisamehewe hata senti tano.

Huu ndio ukarimu na uadilifu unaotakiwa kwa binadamu, ni uadilifu usiokuwa na upendeleo wowote au kumkandamiza mtu wa mbali. Kwani tumeona hapa ni kwa namna gani Mtume (juu yake rehema na amani) ameishi vizuri na mateka mafukara, ambapo walisamehewa pasi na kulipa chochote, lakini kwa upande wa pili alimzidishia malipo Ami yake mwenyewe ambaye alikuwa ni mwenye kipato kikubwa.

Kwa kufanya hivi, Mtume alikuwa akiwafunza wafuasi wake kwamba wawe na uadilifu, huruma na ubinadamu, anasema Mwenyezi Mungu ***mtukufu 'Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.' (19 :107)***

**i.** Miongoni mwa matukio yanayoonesha huruma ya Mtume, ni pale watu wa Makka walipotuma fidia za kuwakomboa mateka wao, na kwa upande wake Zainab binti wa Mtume (juu yake rehema na amani) akiwa Makka aliagiza mkufu (uje Madinah) ili kumtolea fidia mumewe Abi Al-Aasi bin Rabii ambaye pia alikuwa ni mateka. Ikumbukwe kuwa mkufu huu ulikuwa ni zawadi ambayo Bi Khadija (ambaye ni mama wa Zainab) alikuwa amempatia mwanae usiku wa ndoa yake kwa Abii Al-'Aasi, hivyo basi Mtume (juu yake rehema na amani) alipouona mkufu huu alimsikitikia sana Zainab, akasema kama itawapendeza mumuache huru mateka wake na mumrudishie mkufu wake, maswahaba wakasema ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi wakamuacha huru Abii Al-'Aasi na wakamrudishia Zainab mkufu wake.

Huu ni ubinaadamu na upole mkubwa sana. Ni watu wachache sana ambao hulisoma tukio hili kisha wasitokwe na machozi, yote haya ni kwa sababu ya kumsikitikia mwanamke yule maskini ambaye aliamua kuagiza kitu chenye thamani kubwa kwake kwa ajili ya kumtolea fidia mumewe, ni zawadi ambayo alipewa na marehemu mama yake usiku wa ndoa yake, hii inamaanisha kwamba alikuwa hana kitu kingine chenye thamani zaidi ya ule mkufu, hivyo akalazimika kuagiza kitu chenye kumbukumbu kubwa ya mama yake, bali kumbukumbu kubwa ya ndoa yake ili amtolee fidia mumewe. Na kwa upande mwingine, Mtume (juu yake rehema na amani) alipoona mkufu huu alimkumbuka Bi Khadija (Mungu amridhie) na Khadija alikuwa na nafasi kubwa tu kwake katika hali ya uzima wake na hata baada ya kufa, kisha alimsikitikia sana binti yake, lakini pamoja na hayo alitaka ushauri kwa maswahaba zake kama itawapendeza kumrudishia Zainab mkufu wake na kumuacha huru mumewe, nao wakaitikia ombi hili la Mtume (juu yake rehema na amani).

**j.** Al-Nadhri bin Harith alikuwa ni mmoja kati ya Maqureishi wanaoupinga sana Uislamu, bali alikuwa akiwaudhi waislamu pamoja na kuutukana Uislamu wenyewe, sasa vilipozuka Vita vya Badri, alikuwa ni mmoja wa mateka, hivyo Mtume (juu yake rehema na amani) akamuua. Ni vema ikafahamika kwamba, huyu aliuawa si kwa sababu ni mateka, bali ni kutokana na makosa yake mengi ya huko nyuma dhidi ya Uislamu na

waislamu, pamoja na hivyo dada wa marehemu huyu alipojua kuuawa kwa ndugu yake akatunga Kaswida (mashairi) kuhusu kuuawa kwa nduguye. Inasemekana kuwa Mtume (juu yake rehema na amani) ilipomfikia kaswida ile alisema 'lau kaswida hii ingenifikia kabla ya kuuawa kwake, ningemsamehe na kumuacha huru'.

Kuna tukio lingine la ukarimu wa Mtume linafanana na hili, lilitokea katika Vita vya Badri, nalo ni kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliwakataza maswahaba zake wasimuue Al Harith bin Amir bin Nawfal, lakini kwa bahati mbaya kuna mtu alikutana naye akamuua pasi na kujua kwamba huyu ndiye Harith mwenyewe, basi Mtume aliposikia habari hii alisema 'lau ningekutana naye mimi, ningemuacha aishi na wake zake'.

Huyu ndiye Mtume mpole ambaye anawakumbuka na kuwasikitikia mpaka wake wa maadui zake, licha ya kwamba katika mateka hawa kuna wale waliokuwa wakimuudhi Mtume (juu yake rehema na amani) waliobeba mapanga kwa ajili ya kumuua, lakini pamoja na hayo yote, Mtume (juu yake rehema na amani) aliwahurumia na kuwakumbuka watoto na wake zao, kwamba anawasamehe maadui zake kwa kuwahurumia wake zao. Pia tunaweza kuona katika usia wake Mtume amekataza kuwaua watoto wa wasiokuwa waislamu na wanawake zao.

Huruma ya Mtume (juu yake rehema na amani) imeenda mbali zaidi na kuwafikia mpaka ndege katika viota vyao. Mtume alikuwa hakubali kuona mwanajeshi wake anamdhulumu ndege. Ikumbukwe kwamba siku moja Mtume alikuwa akisafiri na maswahaba zake ambao walimuona ndege akiwa katika kiota chake yeye na makinda yake, mtu mmoja katika maswahaba akawachukuwa wale makinda, yule ndege akaja kwa Mtume huku akipiga piga mbawa zake, naye Mtume (juu yake rehema na amani) akasema: 'Ni nani (aliyempa pigo) aliyemuumiza huyu kwa wanawe? Hebu mrudishieni makinda wake'. (Sunan Abu Daud)

Hii ni huruma kubwa sana inayowafikia mpaka ndege, na kwa mujibu wa maelezo ya Mtume, Ni nani (aliyempa pigo) huyu ? kwa muono wa Amiri jeshi huyu mkubwa (Mtume (juu yake rehema na amani) jambo lile ni kumpa maumivu ndege kwa kuchukuliwa makinda wake, ambapo anawaamrisha wanajeshi wake wamrudishe yule kinda katika kiota chake, hii ni huruma ya hali ya juu ambayo haielezeki.

Huruma hii inaweza kufananishwa na vilio vya wajane ambao wanashuhudia watoto wao wakiuawa au kutekwa na habari zao zikipotea moja kwa moja, pasi na kupata moyo unaowahurumia na hisia zinazowakumbuka na wao kupata maumivu kama yale wayapatao.

Hii ni baadhi tu ya mifano ya mambo ya kibinadamu yaliyotokea katika Vita vya Badri, kati ya Mtume (juu yake rehema na amani) na wanajeshi wake na maadui zake. Na ijapokuwa mifano hii inatupa picha ndogo ya namna Mtume (juu yake rehema na amani) alivyokua akiishi kibinadamu katika Vita vya Badri ila picha hii inaakisi ubinadamu wa Mtume katika vita vilivyobaki, na utekelezaji wa kivitendo ni ushahidi mkubwa kuliko sheria za maandiko, kwa sababu maandiko ni nyenzo tu wakati utekelezaji wa sheria ndio lengo, na mara nyingi sheria huwa zinakuja na vifungu vizuri lakini kwa upande mwingine haraka sana huvunjwa pale linapozuka la kuzuka ambapo huwa ndio muda haswa wa kuitekeleza.

Picha hii ndogo ya kivitendo kutoka kwa Mtume (juu yake rehema na amani) haiakisi Maisha ya kibinadamu ya Uislamu nyakati za vita tu peke yake, bali inaakisi mfumo mzima wa maisha ya kawaida, kwani mtu ambaye anamheshimu binadamu wakati wa vita ilhali ni adui yake, mtu huyu bila shaka ataheshimu zaidi haki za binadamu wakati wa amani na ushirikiano. Tunamuomba Mwenyezi mungu atuwafikishe.

# HITIMISHO

Katika hitimisho la tafiti hii napenda kuandika muhutasari wa mambo niliyoyagundua, nayo ni kama ifuatavyo:

1. Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ni msamiati mpya ukilinganishwa na vifungu vya Sheria ya Kiislamu ambayo imeweka na kudhamini haki za binadamu wakati wa migogoro ya kutumia silaha, kwani sheria hii ipo tangu zaidi ya miaka 1400 iliyopita.

2. Kwamba asili ya mahusiano ya Dola ya Kiislamu na mataifa mengine ni kuishi kwa amani, na kwamba vita katika mtazamo wa kiislamu ni jambo la dharura tu, ambalo lengo lake kuu ni kuzuia uadui, kuteteta haki au kuhakikisha uhuru wa kuabudu. Na kwa msingi huu, endapo vita itazuka basi ni lazima kutazingatiwa nyenzo sahihi za utekelezaji wa vita hiyo sambamba na kuheshimu maadili na tabia nzuri.

3. Misingi mikuu ya Sheria ya Umma ya Kimataifa ya Kiislamu ni kwamba binadamu wote ni kitu kimoja ambao wanatakiwa kusaidiana katika mambo ya heri, kusameheana, kuwa na uhuru wa kuabudu, uadilifu na kutendeana kwa wema, kama wanavyopenda kufanyiwa wawafanyie wengine kwa kuzingatia maadili mema. Na kanuni hizi zinatokana na Qur'an na Hadithi pamoja na ada na desturi ambazo hazikinzani na maandiko ya sheria ya kiislamu.

4. Sheria ya Umma ya kimataifa ya kiislamu imethamini sana tabia nzuri, ni kwamba, kama ambavyo ni lazima kuzingatia na kuishi na tabia nzuri kati ya mtu na mtu, vile vile tabia nzuri hizi inatakiwa zizingatiwe zaidi katika mahusiano kati ya mataifa.

5. Sheria ya Umma ya Kiislamu pia imethamini mtu kujilinda yeye mwenyewe (kutii sheria pasi na masharti), basi ni kwa namna hiyo hiyo Uislamu umeitaka Dola ya Kiislamu kutii masharti yenyewe na kutekeleza sheria katika mahusiano yake na nchi nyingine.

6. Tunaweza kufasili Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu kuwa ni mjumuisho wa vifungu vya kisheria vinavyolenga kumlinda binadamu na haki zake katika nyakati za migogoro ya kutumia silaha.

7. Kwamba kuna mambo mawili makubwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu nayo ni :
   a. Inatakiwa vita viwepo kwa kiasi cha dharura tu na si vinginevyo.
   b. Kwamba mambo yanayotokea wakati wa vita yanatakiwa kuzingatia utu na kuheshimu haki za binadamu.

8. Uislamu umenyanyua hadhi ya maadili kwa kuzingatia mwenendo mzima wa binadamu mmoja mmoja na makundi, katika nyakati zote, na hasa hasa inapovuma sauti ya silaha na kufifia sauti ya sheria. Na muda wowote, maadili mema yakiwa ni mambo ya kawaida basi hata haki za binadamu nazo hulindwa na kuthaminiwa, na hapo ndipo utu nao hukirimiwa, na huu ndio msingi mkuu wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu.

9. Katika tafiti hii nimebainisha ulinzi ambao unatolewa kwa majeruhi na waliokumbwa na maafa vitani, na nimeeleza ni kwa namna gani binadamu anatakiwa kupatiwa mahitaji ya lazima, kwani haifai katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu kumuua majeruhi au kumtesa, kama ambavyo haifai kumuacha akiteseka kwa maumivu pasi na kumpatia dawa.

10. Kama ambavyo nimebainisha haki za mateka, huku nikiwa nimeanza kwa wosia wa Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema: ‘wausieni heri mateka’ wosia huu umekusanya kila kitu kizuri cha maneno au vitendo, cha kihisia au kuonekana.

11. Pia nimetaja haki za mateka juu ya kutekeleza ibada zake ilhali bado ni mateka, na kwamba haifai kujaribu kumlazimisha abadili dini yake.

12. Nimebainisha kwamba Uislamu hauwavunjii ahadi mateka, hata kama adui atavunja ahadi dhidi ya mateka wa kiislamu.

13. Pia nimebainisha kwamba mateka ambao ni ndugu haifai kuwatenganisha, hivyo, haifai kuwatenganisha kati ya mama na mwana, au baba na mtoto wake au kati ya ndugu, n,k.

14. Na katika nyanja za haki za mateka, nimetaja kwamba Uislamu umekataza kufanya maamuzi ya mihemko ambayo yanaweza kujitokeza kwa wanajeshi wakati wa kumdhibiti mateka, maamuzi ambayo mara nyingi huwa hayapo sawa, huwa ni matokeo ya jazba na hisia tu zinazopelekea

kwenye dhulma na uadui. Pia nimeweka wazi kwamba jambo la kumhukumu mateka linatakiwa liwe chini ya hakimu na si mwanajeshi, ili kuepuka kutokea kwa jambo lolote ambalo si la kibinadamu na huenda likamdhuru mateka.

**15.** Nimetaja pia kwamba hakimu ana hiari ya hukumu tofauti dhidi ya mateka, ikiwa ni pamoja na kumsamehe au kumuacha huru kwa gharama, kisha nikaeleza kwamba kuna tofauti kati ya wanazuoni kuhusu kumuua mateka, kisha nikataja hoja za pande zote mbili, na kwamba desturi za kimataifa zikionelea kwamba haifai kuua mateka basi na Dola ya Kiislamu itakua mstari wa mbele kupokea maamuzi haya na kuyafanyia kazi, kwa sababu kufanya hivyo kutahakikisha masilahi ya pande zote mbili na kuuheshimu utu wa binadamu.

**16.** Kisha nikataja haki za waliouawa vitani, na namna gani Uislamu unamuheshimu binadamu ikiwa yu hai au maiti, na nikaelezea kwamba moja wapo ya njia ya kumuheshimu maiti vitani ni kuheshimu mwili wake na kumpa heshima yake, na miongoni mwa hayo ni kwamba haifai kumkatakata vipande vipande au kunyofoa kichwa chake.

**17.** Ili kuulinda utu wa binadamu, Sheria ya Kimataifa ya Kiislamu inawataka waislamu kuizika maiti ya yeyote yule pasi na kuangalia dini yake, kama ambavyo inakataza kuicha miili hiyo bila ya kuizika, hii ni kwa sababu ya kumheshimu maiti huyu kwa kuwa ni mwanadamu.

**18.** Kuhusiana na haki za raia wa kawaida nimebainisha kwamba Sheria ya Kimataifa ya kibinadamu ya Kiislamu inawataka wapiganaji kutofautisha kati ya wanajeshi wapiganaji na raia wa kawaida, hii ni pamoja na kutofautisha kati ya kambi za jeshi na vyanzo vya huduma za kijamii, na kwamba haifai kuwagusa kwa ubaya wowote wanawake, wazee, watoto, viongozi wa dini, wakulima n,k, kama ambavyo haifai kushambulia makazi yao na sehemu zao za ibada, au vituo vya tamaduni kama vile maktaba na majengo ya shule na vyuo n,k.

**19.** Kutokana na mwongozo wa kivitendo uliopatikana katika Vita va Badri, imebainika wazi kwamba Mtume alikuwa anapenda kuona kwamba wito wake si maneno tu peke yake, bali alionesha kwamba yeye ndiye mtekelezaji wa kwanza wa kile alicholingania, hivyo maandiko na mwenendo vimeungana pamoja ili kuweka misingi ya kile kinacholinganiwa.

**20.** Unyeyekevu wa Mtume (juu yake rehema na amani) kwa maswahaba zake, kwa namna ambayo alikuwa akionekana yeye ni kama mmoja tu kati yao, na huu ndio msingi hasa wa kuishi vizuri na watu wote na ndio unyenyekevu unaotakiwa kwa viongozi mbele ya wanajeshi wao, ni uadilifu wa nafsi na kuwaheshimu wengine, na pale kiongozi anapoweza kuasisi misingi hii mizuri kwa jeshi lake anakuwa amefanikiwa kuweka misingi ya kushinda mihemko hivyo hataweza kudhulumu wala kuvuka mipaka, vitu hivyo kwake vitakuwa ni mwiko, na hivyo itakuwa heshima yake kwa wengine ni kubwa.

**21.** Muda wowote tutakapoweza kuhurumiana wenyewe kwa wenyewe katika mazingira tofauti, huu utakuwa ni ufaulu mkubwa usio na kifani katika kutekeleza sheria ya kimataifa ya kibinadamu kuliko hata ambavyo sheria yenyewe inatutaka kuifuata, licha ya kwamba hili ndio lengo la sheria ya kimataifa ya kibinadamu.

**22.** Katika Vita vya Badri, wakati naelezea namna Mtume (juu yake rehema na amani) alivyokuwa anaishi na mateka nilitaja mazingatio kadhaa ya kibinadamu ambayo yalibainisha vipi mateka walipata muamala mzuri, kama vile kupatiwa chakula kizuri kuliko cha maswahaba na kwamba mateka walipanda wanyama huku maswahaba wakitembea kwa miguu, na mateka kupewa nguo zinazowapendeza, na wengineo kuachwa huru bure kwa sababu tu ya kuwasikitikia mabinti zao, kwani Mtume (juu yake rehema na amani) alijua kuwa waliwaacha mabinti zao, na mateka wengine kupata kuhudumiwa kama wageni kwa kupakwa mafuta kichwani na kutengenezwa nywele na kuwekwa kwenye nyumba za wenyeji wao.

**23.** Kwa ujumla, tunasoma katika Vita vya Badri vitendo vya upole wa Uislamu katika kuishi na adui vitani, tunamuona mateka na tunaiona taswira ya muamala na ulinzi anaopatiwa.

**24.** Muamala huu tulioushuhudia katika Vita vya Badri, utabaki kuwa mfano na mwongozo tu kwa mtafiti ili apate kuona ni kwa kiasi gani Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa na muamala mzuri katika vita vyake. Na zaidi ya hapo, kujua ni kiasi gani Uislamu unaheshimu utu wa binadamu, ambae anaweza kumuheshimu mtu ambae ni adui yake aliyebeba silaha dhidi yake bila ya shaka ni rahisi na vema zaidi kumfanyia hivyo wakati wa amani na wakati wa ushirikiano.

**25.** Nimebainisha kwamba misingi hii inayotunga haki za binadamu wakati wa vita, ni mafundisho matukufu ya Mwenyezi Mungu na kwamba mwenye kwenda kinyume na mafundisho haya atakuwa na adhabu mara mbili, kwanza adhabu za hapa hapa duniani nayo ni ile adhabu iliyowekwa dhidi ya mwanajeshi anayekiuka sheria, pili ni adhabu ya siku ya kiama, anasema Mwenyezi mungu,
***'Na misiba inayo kusibuni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu. Naye anasamehe mengi.' (42 :30)*** na anasema Mtume (juu yake rehema na amani) *'Wenye huruma, nao Mwenyezi Mungu anawahurumia'* na kinyume chake maana yake ni sahihi.

**26.** Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya Kiislamu imepata himaya kubwa kutoka katika sheria ya Kiislamu na kadhalika imepata dhamana kubwa ya utekelezaji wake; kwa kuzingatia kuwa sheria ya Kiislamu ni sheria kutoka kwa Mwenyezi mungu aliyetukuka, hivyo basi mwenye kwenda kinyume na sheria hii ataadhibiwa mara mbili kama ilivyoelezwa hivi punde, moja ni hapa hapa duniani ambapo atadhibiwa na hakimu na pili ni kesho mbele ya Mwenyezi Mungu. Hili ndilo linalomsukuma muislamu mpiganaji kuhakikisha anatekeleza maelekezo haya, kwani akiweza na kufanikiwa kukimbia adhabu ya duniani hatoweza kukimbia adhabu ya kesho kiama.

Na Mwenyezi Mungu Amrehemu Mtume wetu Muhammad. (Juu yake rehema na amani).

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu huwasaidia waathirika wa vita na vurugu zingine, ikifanya kila iwezavyo ili kulinda hadhi yao na kupunguza mateso wanayopitia, ikishirikiana na washiriki wake wa Red Cross na Red Crescent. Shirika hili pia hujaribu kuzuia taabu kwa kueneza na kukuza sheria za kibinadamu za kimataifa na kutetea kanuni za kimataifa za kibinadamu.

Watu wanafahamu kwamba wanaweza kuitegemea Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu kutoa huduma za kuokoa maisha katika maeneo ya vita na kufanya kazi kwa kushirikiana na jamii zilizoko huko, ili kuelewa na kushughulikia mahitaji yao. Inatambulika kwamba, uzoefu na utaalamu wa Shirika hili umelifanya liweze kukidhi mahitaji kwa haraka, tena kwa ufanisi na bila kuegemea upande wowote.


facebook.com/icrc
twitter.com/ICRC_Nairobi
instagram.com/icrc

**International Committee of the Red Cross**
Nairobi Regional Delegation,
Denis Pritt Road
P. O. Box 73226-00200 Nairobi, Kenya
T +254 20 272 3963
E-mail: nairobi@icrc.org

**International Committee of the Red Cross**
Hamza Aziz Street,
Plot No1736, Block B, Kahama Court-Masaki,
P.O. Box 23431 Dar es Salaam, Tanzania
T: (+255) 222 600 446/7/8/9
E-mail: daressalaam@icrc.org

www.icrc.org

© ICRC, November 2020

1431/400 11.2020 400